SportPesa
JACKPOT BABA LAO!
TZS. 288,541,640
CHEZA SASA KWA 1000/= TU!
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#



**Wanafunzi** walivyofariki dunia kwa kuangukiwa kifusi...
UKURASA 8



**RONALDO AKATALIWA BAYERN MUNICH**
UKURASA 22

Nipashe
Jumatatu Julai 18, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya
ISSN 0856 • Na. 0581010
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US




# Nyuma ya pazia bei nafaka kupaa

UKURASA 2

**2,500**
Bei ya kilo moja ya mchele iliyopo sokoni kwa sasa





**900**
Bei ya kilo moja ya mahindi kwa sasa sokoni.

**2,000**
Bei ya ngano kwa kilo moja sokoni kwa sasa.



**ZILIZOPUNGUA**



Kilo moja ya unga wa mahindi imeanza kushuka

Mafuta ya kula nayo yameanza kupungua bei sokoni.



## YALIYOMO

**UKURASA WA 3**
### UONGOZI WA KIJIJI WADAIWA KUUZA MSITU
WAKAZI wa Kijiji cha Mbika, Kata ya Ushetu wilayani Kahama, wamedai uongozi wa kijiji hicho kuuza msitu wa kijiji bila kuwahusisha na...

**UKURASA WA 4**
### TARURA SINGIDA YAOKOA MIL. 448/- UJENZI DARAJA
WAKALA wa Barabara Mjini na Vijijini (TARURA), Mkoa wa Singida umeokoa Sh. milioni 448 baada ya kujenga daraja katika kijiji cha...

**UKURASA WA 5**
### TEF YATEUA WABOBEZI MAFUNZO MABADILIKO SHERIA ZA HABARI
JUKWAA la Wahariri Tanzania (TEF), limeteua timu ya wataalamu wabobezi wa habari, itakayotoa mafunzo kwa waandishi wa habari...

# PM: Watumishi msing'ang'anie ofisini katatueni kero za wananchi

UKURASA 3




Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi (wa pili kushoto), akifungua pazia ikiwa ni ishara ya kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa Hospitali ya Wilaya wakati wa ziara yake ya kutembelea miradi mbalimbali ya maendeleo katika Wilaya ya Magharibi 'B'. Kulia ni Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui. **PICHA: IKULU**

# Uagizaji mafuta pamoja waondoa ubabaishaji

UKURASA 3

**MICHEZO** TFF YAFUNGIA VIWANJA SABA UK.24 | **MAONI, KATUNI** UK.6

# Nyuma ya pazia bei nafaka kupaa

Na Waandishi Wetu

LICHA ya serikali kuendelea kudhibiti kupanda kwa bei ya chakula kwa kuweka mikakati kuhakikisha kunakuwapo na chakula cha kutosha nchini, bei za nafaka zimeendelea kupanda huku wauzaji wa rejareja wakiwatupia lawama wauzaji wa jumla kwa kupandisha bei za bidhaa hizo mara kwa mara.

Nipashe imetembelea baadhi ya wafanyabiashara wa chakula wa jumla ili kujua kinachosababisha bei ya bidhaa hiyo kupanda mara kwa mara licha ya serikali kuweka juhudi mbalimbali kuidhibiti.



Bidhaa za nafaka zikiwa sokoni. **PICHA: MTANDAO**

**DAR ES SALAAM**

George Mashaka (45), mfanyabiashara wa mchele kwa jumla katika Soko la Temeke, alisema kupanda kwa bei ya bidhaa hiyo kunachangia mfumuko wa bei ya vyakula, pia upatikanaji wa bidhaa hiyo umekuwa mgumu kwa sasa kutokana na wakulima wa ndani kuangalia zaidi masoko ya nje ya nchi kwa ajili ya maslahi yao.

Alisema kwa sasa mchele ulipaswa kuuzwa kwa bei ya chini kwa kuwa ni miezi ya mavuno, akirejea kumbukumbu zake za miaka miwili iliyopita kipindi kama hiki bidhaa hiyo ilikuwa inapatikana kwa bei ya kuanzia Sh. 1,200 kwa bei ya jumla, lakini sasa wanauza kuanzia Sh. 1,800 kwa kilo.

Mfanyabiashara huyo alisema kwa sasa wanalazimika kununua mchele huo kwa gharama sawa na wanunuzi wa nje ya nchi kwa kuwa bila kufanya hivyo, bidhaa zote zitakwenda kwenye nchi zao, zikiwamo Kongo, Rwanda, Burundi na Uganda na wao kutofanya biashara.

"Soko hili sasa hivi limevamiwa na wafanyabiashara kutoka nchi za nje. Ukienda sasa hivi Mbeya, utakuta wafanyabiashara wa Kongo wamejaa, ukienda Mpanda na Kanda ya Ziwa, unakuta wafanyabiashara kutoka Burundi na Uganda wamejaa, ambao sasa hivi wanakwenda moja kwa moja shambani kununua mpunga badala ya kwenda kwenye mashine.

"Tena kama wewe ulikuwa ununua gunia kwa Sh. 40,000, mwenzako ananunua kwa Sh. 60,000. Sasa mkulima si atamuuzia Mganda?" George aliwasilisha uzoefu wake.

Alisema hali hiyo imesababisha wafanyabiashara wa ndani kupandisha bei ya bidhaa hizo, huku akikiri biashara yao hiyo kwa sasa ni ngumu kwa sababu wamepoteza wateja, na katika kukabiliana nayo, wanalazimika kuuza kwa bei ya rejareja ili kufikia malengo yao.

"Zamani tulikuwa tunauza mchele kuanzia kilo 10 kwa kuwa tulikuwa tunauza Sh. 1,200 hadi 2,000 kwa kilo, lakini sasa jeuri hiyo baadhi yetu hatuna. Ni kwa sababu mchele huo huo tunauza kwa Sh. 1,800 hadi 2,500, wateja wamepungua. Kwa hiyo, sasa akija mtu akitaka kilo moja tunamuuzia, mradi na sisi tupate riziki," alisema.

Mfanyabiashara wa jumla wa maharagwe katika soko hilo, Rashid Ahmad, alisema mbali na soko la bidhaa hizo kuvamiwa na wafanyabiashara kutoka nje ya nchi, mwaka huu mavuno yamekuwa kidogo na upatikanaji wake umekuwa wa shida na wakulima kupandisha bei ili kupata faida zaidi.

Ahmad alisema kupanda kwa gharama za usafirishaji pia kumekuwa kikwazo kwao, hivyo wanalazimika kupandisha bei ili kufidia ongezeko la gharama za usafirishaji.

"Hawa wenzetu (nchi jirani) inaonekana mwaka huu kama hawakulima kabisa kwa sababu wamejaa sana nchini na wananunua kwa bei ya juu tofauti inayotambulika.

"Kwa hiyo, inabidi na sisi tufike bei hiyo ili tupate bidhaa, lakini itambulike pia kwa sasa kusafirisha gunia la kilo 100 kutoka Makambako hadi hapa Temeke ni Sh. 10,000 kutoka Sh. 6,000 ya awali. Sasa hatuna jinsi, lazima na sisi tupandishe bei," alifafanua.

**SHINYANGA**

Mfanyabiashara Alex Paulo wa mkoani Shinyanga, aliiambia Nipashe mwishoni mwa wiki kuwa kilo moja ya maharagwe kwa sasa wanaiuza Sh. 2,400 kwa kuwa wananunua gunia la kilo 100 kwa Sh. 220,000 tofauti na awali bei ilikuwa Sh. 160,000 hadi 170,000.

Wakati bei ikiwa juu kwenye baadhi ya maeneo nchini, mfanyabiashara wa unga wa mahindi kwa bei ya jumla katika Soko la Tandale aliyejitambulisha kwa jina la Big, alisema kwa sasa bidhaa hiyo imeanza kupatikana kwa wingi na wameshuhudia kushuka kwa bei na anaamini kama hali hiyo itaendelea, gharama zitarudi kama zamani.

"Tuna wiki sasa mahindi yameanza kuja kwa wingi, kidogo gharama zimeshuka huko tunakonunulia na sisi tumeshusha. Sasa hivi kiroba cha kilo 25 tunauza Sh. 35,000 kutoka Sh. 38,000.

"Kiroba cha kilo 10 tunauza Sh. 15,000 kutoka Sh. 17,000 na kilo tano tunauza Sh. 7,000 kutoka Sh. 8,000 tuliyokuwa tumefikia hivi karibuni," alifafanua.

Hali hiyo ni tofauti kulinganisha na baadhi ya mikoa ikiwamo Arusha, mahindi yameonekana bado yanauzwa bei juu.

**ARUSHA**

Elizabeth Mafwere, mfanyabiashara katika Soko la Kikatiti lililoko wilayani Arumeru mkoani Arusha, alisema kwa sasa wananunua gunia la mahindi kwa Sh. 100,000 na wao wanawauzia wanunuzi wa jumla kwa Sh. 105,000, akifafanua kuwa ni ongezeko kubwa kulinganishwa na miaka iliyopita.

"Tulizoea msimu huu wa mavuno na mahindi yakiwa mapya gunia tulinunua kwa Sh. 30,000 hadi Sh. 40,000, hali imekuwa ni tofauti sana mwaka huu, kwa sasa ndio kwanza wakulima wanaanza kuvuna kile kidogo alichopatikana," alisema Mafwere.

Alphonse Charles, dalali wa mchele jijini Arusha, alisema kuwa kitendo cha wafanyabiashara wa nje kununua bidhaa kwa wakulima kwa bei ya juu, bei inakuwa juu kwa sababu hata wanunuzi wa ndani nao wanakwenda kufuata bidhaa hiyo mikoani kwa wakulima.

"Ina maana bei kule kwa wakulima inapopanda, inabidi na sisi huku tuje kupandisha, na hawa nao wamekuwa wajanja, sasa hivi wanakwenda wenyewe mashambani au mashineni huko kununua mchele, sasa hapo na sisi pia tunaathirika maana wateja wamepungua sana," alilalamika.

**TANGA**

Mkoani Tanga, Nipashe imeshuhudia katika baadhi ya maeneo unga wa ngano umepanda kutoka Sh. 1,500 kwa kilo hadi Sh. 2,000 huku unga wa mahindi nao ukielezwa kupanda kutoka Sh. 1,000 kwa kilo mpaka Sh. 1,500.

Katibu wa Soko Kuu la Mgandini jijini Tanga, Shabani Mohamed, alisema magari yaliyokuwa yakipeleka bidhaa kwenye soko hilo, yamepungua kutokana na bidhaa kupanda bei na kusababisha baadhi ya bidhaa kuadimika.

**DODOMA**

Makao Makuu ya nchi mkoani Dodoma, Meneja wa Soko la Kimataifa la Mazao la Kibaigwa mkoani Dodoma, Emanuel Kereyani, alisema msimu huu bei ya mazao hasa mahindi imepanda hadi kufikia Sh. 820 kwa kilo kwa sasa.

"Bei ya mahindi kwa sasa inapanda badala ya kushuka. Wakati msimu ulipoanza, kilo moja ilinunuliwa kwa Sh. 600 lakini sasa yanapanda tu, yamefika Sh. 820 kwa kilo kwa saa na kuna wakati yalifika hadi Sh. 900 kwa kilo lakini baadaye yalishuka na kufikia hii Sh. 820," alisema.

Kiongozi huyo alisema alizeti kilo moja sasa inauzwa Sh. 1,000, mtama mweupe na mwekundu gharama yake ni Sh. 620 hadi 650 kwa kilo.

"Hizi bei tukilinganisha na misimu iliyopita zipo juu sana, tangu soko lianzishwe haijawahi kutokea, mwaka huu bei ni kubwa sana, misimu mingine iliyopita kilo tulikuwa tunanunua hata kwa Sh. 350," alisema.

Nipashe ilipohoji kuhusu wafanyabiashara wa nje kununulia mazao mashambani, meneja huyo alikiri kuwapo hali hiyo, akisema wameingia kwa kasi huko vijijini na wananunua kwa bei kubwa.

"Kwenye soko letu hatuna uhaba mkubwa kwa sababu mazao yanaingia kila siku, kwa sasa tupo kwenye msimu wa mahindi, yanaingia kwa wingi lakini bei imekuwa kubwa," alisema.

Mwenyekiti wa Soko Kuu la Majengo jijini Dodoma, Godson Rugazama, alisema hali ya upatikanaji wa mazao katika soko hilo ni mbaya huku bei zikiendelea kupanda kila siku.

Alisema kiroba ya unga wa mahindi cha kilo 10 ambacho mwaka jana kipindi kama hicho kilikuwa kinaunzwa Sh. 17,000, mwaka huu kinauzwa Sh. 38,000, ikiwa ni zaidi ya mara mbili ya bei ya mwaka jana.

**MIKAKATI NFRA**

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA), Milton Lupa, alisema wakala unaanza kununua mahindi kwenye mikoa mbalimbali na kwamba bei itazingatia hali ya mikoa husika.

Alisema wamepanga kununua tani 100,000 za nafaka. Kati yake, mahindi tani 95,000, mpunga tani 4,000 na mtama tani 1,000.

Alisema na wanakwenda kununua katika mikoa ya nyanda za juu kusini ambayo ndiyo ina chakula kwa wingi, huku akikiri uzalishaji wa mwaka huu umeshuka kulinganisha na ule wa mwaka jana.

Ofisa huyo alisema kuwa kabla ya kununua, wanajiridhisha kwanza kuhusu usalama wa chakula nchini.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alipowasilisha bungeni hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka huu wa fedha, alitaja vipaumbele vyao ikiwa ni pamoja na kujitosheleza kwa mahitaji ya chakula ndani ya nchi na kuuza nje ya nchi.

Bashe pia alisema watafanya mwelekeo wa uzalishaji wa mazao ya chakula kuwa wa kibiashara, akibainisha kuwa wataongeza mauzo ya mazao nje ya nchi kutoka Dola za Marekani bilioni 1.2 hadi Dola za Marekani bilioni tano ifikapo mwaka 2030.

**MBEYA**

Mkoani Mbeya, Nipashe ilitembelea masoko mbalimbali ya Jiji la Mbeya na yaliyopo katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi kwa ajili ya kuangalia bei za mazo hayo na upatikanaji wake ambapo wafanyabiashara wa mazao hayo walisema kwa sasa kila zao limepanda bei.

Katika Soko la Mbalizi mahindi yanauzwa kwa bei ya kati ya Sh. 13,000 na 15,000 kwa debe, huku wafanyabiashara wakieleza kuwa upatikanaji wa nafaka hizo ni wa shida kwa sasa.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Rhoida Sanga alisema licha ya bei ya nafaka hizo kuwa nzuri kwa sasa,

INAENDELEA UK. 4



Mtoa huduma wa Asasi ya Vodacom Tanzania Foundation, Fatma Samwel (katikati), akitoa maelezo kuhusu huduma mbalimbali zitolewazo na asasi hiyo kwa wanafunzi wa shule ya awali ya Grastaiva kutoka Mkuranga, walipotembelea banda la asasi hiyo katika maonyesho ya 46 ya biashara ya kimataifa ya Dar es Salaam yaliyomalizika wiki iliyopita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# PM: Watumishi msing'ang'anie ofisini katatueni kero za wananchi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka watumishi wanaopenda kung'ang'ania kukaa ofisini watoke kwenda kufanya mikutano na wananchi vijijini kwa ajili ya kusikiliza kero zao na kuzipatia ufumbuzi.

Akizungumza na wananchi wa Kata ya Nduguti wilayani Mkalama baada ya kuzindua jengo la ofisi ya Mkuu wa wilaya katika mwendelezo wa ziara yake ya kikazi mkoani Singida, Waziri Mkuu alisisitiza suala hilo pia alipoongea na watumishi wa Halmashauri za Wilaza za Iramba, Manyoni na Itigi.

Alisema hakuna sababu kwa watumishi kutoa mwanya kwa wananchi kufikia ofisini kuleta kero zao.

"Msitoe mianya ya wananchi kuja sana ofisini, tunawaadhibu mno wanatembea umbali mrefu, wengi wao hawana nauli wanatembea miguu, tuwafuate," alisema.

"Nendeni vijijini, wafuateni wananchi vijijini mkasikilize kero zao wahudumieni huko huko, ofisini ni mahali pa uratibu tu kazi zote zipo vijijini."

Akizungumzia kuhusu maji, aliziagiza Kamati za Mazingira za Vijiji na Kata kuweka utaratibu wa kuzuia kulima na kukata miti kwenye vyanzo vya maji.

Alisema serikali inatumia gharama nyingi kwa ajili ya miradi ya maji na hivi karibuni Rais alitoa Sh. milioni 500 kwa Mkoa wa Singida kwa ajili ya Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi na Mazingira Vijijini (RUWASA), kufanya utafiti kwenye vyanzo hivyo.

"Mnatupa shida ya kutafuta maji watu wanapeleka mifugo na kulima kwenye vyanzo na kuviharibu, tukiendelea na utaratibu huu vyanzo vyote vitatoweka," alisema.

Awali, Meneja wa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) Mkoa wa Singida, Hadija Abdallah, akitoa taarifa ya ujenzi wa jengo la ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mkalama, alisema limegharimu Sh. bilioni 1.3 hadi kukamilika kwake.

Alisema ujenzi wa jengo hilo lenye ofisi 19 ulianza mwaka 2018 baada ya kutengewa fedha katika bajeti ya 2017/2018 na mkandarasi ameshalipwa Sh. bilioni 1.2.

# Uongozi wa kijiji wadaiwa kuuza msitu

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKAZI wa Kijiji cha Mbika, Kata ya Ushetu wilayani Kahama, wamedai uongozi wa kijiji hicho kuuza msitu wa kijiji bila kuwahusisha na kusababisha uvunaji wa miti holela.

Wameiomba serikali kuingilia kati uvunaji huo unaodaiwa kutekelezwa na viongozi wa kijiji, ili kudhibiti uharibifu wa mazingira na viumbe hai na wanyama wanaopatikana kwenye msitu huo.

Malalamiko hayo waliyatoa jana kwenye mkutano wa hadhara uliotishwa na Mbunge wa Jimbo la Ushetu, Emmanuel Cherehani, kwa ajili ya kusikiliza na kutatua kero zinazowakibili wananchi kwenye sekta ya afya, maji, elimu, kilimo na miundombinu ya barabara.

Mkazi wa kijiji cha Mbika, Dalali Bundala, alisema uvunaji na uuzaji wa msitu unaomilikiwa na kijiji hicho, viongozi hawakushirikisha wananchi mpaka walipobaini na kuona usafirishaji mkubwa wa magogo ukiendelea na wanapohoji hakuna majibu sahihi waliyopata.

Alisema kilichofanywa na wananchi hao siyo cha kiungwana, kwa kuwa wananchi walipaswa kushirikishwa hatua zote kupitia mikutano ya kijiji ambayo iko kisheria badala ya kujichukulia sheria mkononi kama walivyofanya sasa.

"Sisi tunashauri mchakato wa uuzaji wa msitu huu usitishwe na serikali iliingilie kati jambo hilo...haiwezekani viongozi wauze miti ya asili 5,000 iliyopandwa na kutunzwa kwa zaidi ya miaka 50 iliyopita bila kushirikisha wananchi," alisema Bundala.

Naye, Diwani wa Ushetu, Pili Sonje, alikiri kutoshirikishwa katika uvunaji na uuzaji wa msitu huo, serikali ya kijiji ilikaa na kukubaliana kuuza msitu huo bila ya kushirikisha kamati ya maendeleo ya kata kinyume na taratibu zinavyotaka na ukihoji viongozi wanakuwa wakali.

Akijibu malalamiko hayo Mwenyekiti wa kijiji hicho, Faida Lutege, alisema uvunaji na uzwaji wa msitu huo alishirikisha wananchi na baadhi ya viongozi wake na kupewa kibali na Wakala la Misitu Tanzania (TFS) wilaya kwa ajili ya kuvuna na kuuza kisheria.

Alisema serikali ya kijiji ilikubaliana na kuwashirikisha wananchi ili kuuza msitu huo kwa ajili ya kujenga ofisi ya kijiji kwa makubaliano kuuza miti 5,000 kwa gharama ya Sh. 4,000 kwa kila mti mmoja, na walitarajia kupata Sh. milioni 20 baada ya kuuza miti yote na kujenga ofisi.

Aidha, Lutege alidai kuwa mpaka sasa wameuza miti 2,000 kati ya 5,000 na ofisi yake imeshapokea kiasi cha Shilingi milioni nane kutoka kwa mzabuni, ambaye amepewa kandarasi ya kuvuna msitu huo wa asili ili kujenga jengo la ofisi ya kijiji cha Mbika.

Kwa upande wake, Mbunge wa jimbo la Ushetu, Emmanuel Cherehani, aligiza kusitishwa kwa uvunaji wa msitu huo na kuagiza magogo yaliyovunwa yasisafirishwe mpaka uchunguzi ufanyike ili kujiridhisha kama sheria ilifuatwa.

Cherehani alisema mpaka sasa ofisi yake haina taarifa za uvunaji wa msitu huo na zaidi ya magogo 2,000 tayari yamekwisha uzwa na kusafirishwa kinyume na matakwa ya wakazi wa kijiji hicho, ni budi zoezi hilo likasimama ili kupisha uchunguzi.

# Uagizaji mafuta pamoja waondoa ubabaishaji

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imetetea umuhimu wa uwapo wa Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA), kwamba unasababisha nchi kuwa na uhakika wa mafuta tofauti na ilivyokuwa zamani kwa kila mtu kuagiza kivyake.

Wakala PBPA inaratibu mfumo wa uagiza mafuta kwa pamoja (BPS), kisha kampuni inayoshinda zabuni ndiyo inayopewa kazi ya kuagiza mafuta ya kampuni zote kutoka mataifa yanayozalisha.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Mhandisi Modestus Lumato, alitoa ufafanuzi huo alipokuwa akizungumza na wahariri na waandishi wa habari wa vyombo mbalimbali, mwishoni mwa wiki.

Alisema utaratibu wa zamani wa kila kampuni ya mafuta kuagiza mafuta kivyake haukuwa ukitabirika na ungeweza kuiingiza nchi kwenye matatizo makubwa ya ukosefu wa nishati hiyo, iwapo ungeachwa uendelee kufanyika holela.

Kwenye utaratibu wa zamani kampuni zilizokuwa zikiagiza mafuta, alisema zilikuwa zikifanya ujanja na ubabaishaji kwa ajili ya kujipatia maslahi zaidi, ikiwamo kuyaficha ili kusubiri bei ipande.

Lumato alisema kwa utaratibu wa sasa hakuna mfanyabiashara anayeweza kufanya ujanja wowote, kwa kuwa serikali inajua kiasi cha mafuta kilichoagizwa na ambacho kila kampuni inapaswa kuchukua baada ya mzigo kuwasili nchini.

Awali, uagizaji wa mafuta ulikuwa ukifanywa na Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC), lakini baada ya kelele nyingi za baadhi ya wafanyabiashara serikali iliamua kuliondoa shirika hilo na likaendelea na shughuli zake za awali.

"Serikali iliamua kuiondoa TPDC kwenye shughuli za uagizaji wa mafuta na kurejesha mfumo wa zamani wa kila kampuni kuagiza, lakini kilichofuata ni ujanja ujanja wa watu ambao wako tayari kufanya lolote ilimradi wapate faida kubwa bila kujali maslahi ya taifa," alisema Lumato.

"Ilifika wakati serikali inashindwa kujua iwapo mafuta yameagizwa au la, kama yameagizwa yamefikia wapi na ni kiasi gani kinakuja, sasa hii ni hatari sana kwa nchi kwasababu waagizaji binafsi wakiamua wasiagize inakuwaje ndiyo sababu ikaja na utaratibu huu ambao unatabirika tunajua tunaleta mafuta kiasi gani, yamefikia wapi na yatatumika mpaka lini," alifafanua Lumato.

Alisema meli za mafuta yanayoagizwa kwa mfumo wa BPS zinapowasili bandarini Dar es Salaam na mzigo huo kila kampuni inawekewa kiasi chake kwenye matangi yake na kisha kuweka alama kwa mafuta ambayo yanasafirishwa kwenda nje ya nchi.

"Mfumo huu ni mzuri sana na mtusaidie kuelimisha wananchi kwa sababu inawezekana kuna watu wanaupinga kwa kutokujua, lakini una manufaa makubwa kwa mfano sasa hivi tuna uhakika wa mafuta hadi Septemba tunajua yanakuja kiasi gani, yamefikia wapi na yanatoka nchi gani," alibainisha.

Kuhusu watu wanaolalamikia zabuni, Lumato alisema hakuna uwezekano wowote wa mzabuni kushinda kwa kutoa rushwa, kwa kuwa zabuni hiyo imekuwa ikiendeshwa kwa uwazi mkubwa.

NGOMENI ENTERPRISES

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA NA NOTISI YA KULIPA DENI**

Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na crdb Plc makao makuu Dar es salaam, tunatoa notisi ya siku kumi na nne(14) tu ili uweze kulipa deni lote unalodaiwa. Kukaidi au kushindwa kulipa deni hilo tutauza dhamana uliyoweka kwa mnada wa hadhara kama inavyoonesha kwenye jedwari hapo chini.

| S/N | JINA LA MTEJA | DHAMANA/MAHALI | TAREHE/MUDA |
|---|---|---|---|
| 1. | PAUL CHARLES KAWONGA | Nyumba - Plot No. 1257Block B, Kinyerezi | 4.8.2022 saa 2 asubuhi na kuendelea |
| 2. | ROBERT SHEDRACK SHAO | Pikipiki Reg. No. MC 824CQU, MC226 CHF, MC 605 CEQ,MC 813 CQU, MC 744 CLA, MC 817 CLA, MC 704 CER, MC 463 CGJ,MC308 CGJ, MC 643 CER, MC427CGJ, MC 820CQU | 5.8.2022 saa 2 asubuhi na kuendelea. |
| 3. | CHRISTINA SAMWEL JENERALI | Chanika -kinyamwezi | 9.8.2022 saa 3 asubhi na kuendelea |

**MASHARTI YA MNADA.**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atakayeshinda atalipa malipo ya 25% ya bei itakayofikiwa siku yam nada na 75% atalipia ndani ya siku 14.
3. Mnuniuzi atakayeshundwa kumalizia salio la 75% katika muda uliopangwahapo juu, hatarudishiwa fedha alizolipa awali na mnada utarudiwa siku nyingine itakayopangwa.
4. Gharama zote za kubadilisha hati miliki,kutwaa nyumba na gharama nyinginezo zitzkuwa juu ya mnunuzi.
5. Wateja wote mnakaribishwa kuona na kukagua dhamana hizo muda wowote isipokuwa usiku.

**MAWASILIANO:**
**CRDB BANK PLC HEAD QUARTER,**
**NGOMENI ENTERPRISES, DSM.**
**SIMU 0719974916/0784252048**

# TARURA Singida yaokoa mil. 448/- ujenzi daraja

**Na Thobias Mwanakatwe,**
MKALAMA

WAKALA wa Barabara Mjini na Vijijini (TARURA), Mkoa wa Singida umeokoa Sh. milioni 448 baada ya kujenga daraja katika kijiji cha Lukomo wilayani Mkalama kwa kutumia teknolojia mpya ya mawe.

Daraja hilo lilizinduliwa jana na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na Meneja wa TARURA Mkoa wa Singida, Tembo David, alisema kwa kutumia teknolojia mpya ya kujenga kwa mawe limegharimu Sh. milioni 102.

"Daraja hili kama tungelijenga kwa kawaida njia ya kawaida lingeigharimu serikali Sh. milioni 550, lakini kwa kutumia teknolojia hii ambayo ni nafuu sana inatumika nchini Hispania na hapa nchini madaraja kama hayo yamejengwa Kigoma na Mbeya," alisema.

David alisema ujenzi wa daraja hilo lenye urefu wa mita 30 na upana wa mita saba, ulianza Desemba 18, 2021 na kukamilika Julai 18, 2022.

Aliishukuru serikali kwa kuongeza bajeti ya ujenzi wa barabara katika Mkoa wa Singida kutoka Shilingi bilioni sita hadi kufikia Sh. bilioni 23.4.

Waziri Mkuu, Majaliwa, aliwapongeza mainjinia kwa ubunifu huo mpya wa ujenzi daraja hilo na kutaka teknolojia hiyo isambae katika mikoa yote nchini.

"Kupitia vikao vyenu vya TANROAD na TARURA hii taaluma muifikishe kwa mainjinia ili kila injinia kwenye mkoa wake atafute fursa na bahati nzuri mawe yamejaa kwenye maeneo yetu," alisema.

Majaliwa alisema serikali imekuwa ikigharamia fedha nyingi kujenga madaraja kwa gharama kubwa wakati kuna Watanzania wabunifu wenye taaluma zao wanaweza kujenga madaraja kwa gharama nafuu.

"Daraja hili hapa miaka yote tulishindwa kulijenga sababu ya gharama na ilikuwa lazima tupate zaidi ya Sh. milioni 500 kumbe mainjinia wetu na usomi wao wana uwezo wa kujenga daraja la kudumu kwa gharama nafuu," alisema.

Naye Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange, alisema serikali imekubaliana na wahandisi wa TARURA kuendelea kuwa wabunifu na kwamba Wilaya ya Mkalama imeongezewa bajeti ya ujenzi wa barabara kutoka Sh. milioni 600 hadi kufikia Sh. bilioni 2.2.




Balozi wa Uturuki nchini Tanzania, Dk. Mehmet Gulluoglu's, akionyesha picha za matukio mbalimbali ya machafuko yaliyotokea nchini Uturuki Julai 15, 2016 na kusababisha vifo vya zaidi ya watu 251 katika hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Taifa hilo pamoja na balozi zake zilizoko nchi mbalimbali duniani huadhimisha siku hiyo kila mwaka. **PICHA: MAULIDI MMBAGA**

# Uturuki yawakumbuka waliouawa jaribio la mapinduzi

**Na Maulid Mmbaga**

UBALOZI wa Uturuki nchini Tanzania umeadhimisha Siku ya Machafuko ya Uvamizi uliokusudia kufanya mapinduzi yaliyotokea Julai 15, mwaka 2016, nchini humo na kusababisha vifo vya watu 251.

Taifa la Uturuki likishirikiana na balozi zake zilizoko katika nchi mbalimbali duniani huadhimisha siku hiyo kila mwaka ifikapo Julai 15, Balozi wa Uturuki nchini, Dk. Mehmet Gulluoglu's aliadhimisha siku hiyo juzi jijini Dar es Salaam.

Wanadiplomasia raia wa Uturuki wanaoishi nchini, baadhi ya Watanzania kama wageni waalikwa na wawakilishi wa balozi mbalimbali ikiwamo Pakistan na Palestina, walihudhuria kumbukizi hiyo. Dk. Gulluoglu's, alisema Julai 15 ni alama ya kigaidi ya kushindwa kwa jaribio la mapinduzi lililofanyika nchini kwake ambalo lilisababisha taharuki na uvunjifu wa amani.

"Jaribio hilo lilisababisha vifo vya Waturuki ambao walijaribu kutetea mapenzi yao ya kitaifa, tutaendelea kuwakumbuka na kulaani wote waliohusika na machafuko hayo," alisema Gulluoglu's.

## Nyuma ya pazia bei nafaka kupaa

INATOKA UK. 2

lakini wakulima wengi hawapeleki kwenda kuuza wakisubiri ipande zaidi na kwamba baadhi yao walivuna kidogo hali ambayo inawafanya wasiuze.

Alisema miaka mingine kipindi kama hiki ambacho wakulima wengi wanakuwa wametoka kuvuna walikuwa wananunua kwa bei ya kati ya Sh. 4,000 na 6,000 kutokana na kuwa mengi, lakini mwaka huu ni tofauti.

"Mwaka jana kipindi kama hiki tulikuwa tunanunua debe moja Sh. 5,000 na kuuza 6,000, lakini mwaka huu tunanunua Sh. 13,000 mpaka 14,000 na tunauza Sh. 15,000 lakini bado hayaonekani," alisema Rhoida.

Naye Sophia Mwakagali, ambaye ni mfanyabiashara wa maharagwe alisema kwa sasa wananunua kati ya Sh. 28,000 na 38,000 kwa debe kulingana na aina ya mbegu na ubora wa mazao yenyewe.

Alisema baadhi ya maharagwe yakiwamo aina ya Kigoma yanauzwa bei kwa sababu yanahitajika zaidi sokoni kutokana na kutumiwa na watu wote wakiwemo hata wenye vidonda vya tumbo.

Alisema maharagwe ambayo yanauzwa bei ya chini ni Rosekoko ambayo ndiyo wananunua Sh. 28,000 na kwamba wao wakiuza huwa wanaongeza kati ya Sh. 1000 na 2000 ili wapate faida.

Katika baadhi ya mashine za kukoboa mpunga na kulikutwa mchele ukiuzwa kati ya Sh. 35,000 na 42,000 na wafanyabiashara walisema bei hizo hutofautiana kulingana na aina ya mpunga na kiwango cha ubora baada ya kukobolewa.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Salome Mzopola alisema mwaka huu mpunga sio mwingi kama ambavyo inakuwa miaka mingine kutokana na mvua kuisha mapema hasa katika Bonde la Kamsamba wilayani Momba ambako ndiko wanatoa asilimia kubwa ya mpunga unaoouzwa Mbalizi.

■ **Imeandaliwa na na Jenifer Gilla (Dar), Richard Makore (Mwanza), Allan Isack, Tumaini Mafie (Arusha), Jaliwason Jasson (Manyara), Oscar Assenga (Tanga), Restuta Damian (Bukoba), Happy Severine (Simiyu), Marco Maduhu (Shinyanga), Renatha Msungu Paul Mabeja (Dodoma), na Nebart Msokwa.**

HABARI KITAIFA



Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe (katikati), akielezewa jambo na Mkurugenzi wa Uzalishaji wa Kiwanda cha Tumbaku cha Alliance One Tanzania, David Mayunga, alipotembelea kiwanda hicho, mkoani Morogoro mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Mkurugenzi Mkuu wa kiwanda hicho, Ephraim Mapoore. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yaahidi kuvilinda viwanda vya uwekezaji

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

SERIKALI imeahidi kuvilinda viwanda nchini ili uwekezaji uliofanyika unakuwa na tija na endelevu.

Kadhalika, itatumia vyema sera, sheria na taratibu za kibiashara kuwezesha uwekezaji uliopo unakua endelevu.

Waziri wa Viwanda na Biashara, Ashatu Kijaji, alitoa ahadi hiyo, alipokuwa na Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, kwenye ziara ya Kiwanda cha Kusindika Tumbaku cha Alliance One Tanzania, kilichoko Morogoro mwishoni mwa wiki.

Alisema wamefurahishwa na uwekezaji mkubwa uliopo na kuwahakikishia wawekezaji kwamba kiwanda chao na vingine nchini vinalindwa na kuwa endelevu.

"Sijawahi kufikiria kuwa kiwanda hiki ni kikubwa kama nilivyokishuhudia leo, nilidhani ni kiwanda kidogo tu," alisema Dk. Kijazi.

Alisema yeye na mwenzake Bashe wamefurahishwa na ukubwa wa uwekezaji na idadi ya wafanyakazi ambao kampuni hiyo imeajiri.

Kiwanda hicho kina wafanyakazi 350 wa kudumu pamoja na wafanyakazi 3,000 wa msimu kwa kila mwaka.

Alihakikisha wizara yake inajitahidi kiwanda hicho kinapata malighafi ya kutosha ili itumie kwa ukamilifu uwezo wake wa usindikaji.

"Rais Samia Suluhu Hassan kila mara anasisitiza haja ya kulinda viwanda hivi kwa gharama yoyote, hivyo tunakuomba utuwasilishie mambo yote ambayo yanakwamisha juhudi za kuwa na uwekezaji endelevu," alisema Dk. Kijazi.

Kwa upande wake Waziri Bashe, aliziasa kampuni za kilimo cha tumbaku na mnyororo wake wa thamani kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za kilimo hicho kama zilizoainishwa kwenye sheria mama ya zao la tumbaku.

"Tunawataka kampuni zote zizingatie sheria, kanuni na taratibu zote zilizowekwa katika sheria ya tumbaku, kuanzia na namna bora ya kuingia mikataba ya ununuzi wa tumbaku na wakulima mpaka utunzaji, uhifadhi wa mazingira kwa maana ya kupanda miti ya kukaushia zao hilo," alisema Bashe.

Kwa kampuni mpya, alisema sheria inawataka kuanzia kwenye kuingia mikataba na wakulima kabla ya kuanza ununuzi wa zao na wanaweza kufanya hivyo kwa kwenda kulifufua zao kwenye vyama vya ushirika ambavyo kwa namna moja au nyingine viliacha kulima zao hilo.

"Kwa vile tunataka kuongeza uzalishaji kutoka kilo milioni 70 za sasa hadi zaidi ya kilo milioni 150, tunatakiwa tufike huko kwa utaratibu na sio kwa vurugu na nataka Bodi ya Tumbaku iwe na msimamo katika hili," alisema Bashe.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, Ephraim Mapoore alisema kuna changamoto kadhaa zinazokabili kampuni yake, lakini kubwa ni kodi waliyonayo na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Alisema katika hilo wana njia mbili, walilipe kodi hiyo au wafunge biashara.

Pia alizungumzia tatizo la umeme na ukosefu wa maji kutoka MORUWASA na kwamba kwa sasa wanategemea visima vyao vya maji na bwawa.

Aliomba kupatiwa njia maalumu ya umeme kwa kuwa sasa wanatumia lita 600 za dizeli kwa siku kuzalisha nishati ya kuendesha kiwanda hicho.

Alliance One ilifungua kiwanda chake cha usindikaji mwaka 1998 na imekuwa ikifanya kazi kwa mafanikio tangu wakati huo bila kukosa msimu wowote.

# TEF yateua wabobezi mafunzo mabadiliko sheria za habari

**Na Mary Geofrey**

JUKWAA la Wahariri Tanzania (TEF), limeteua timu ya wataalamu wabobezi wa habari, itakayotoa mafunzo kwa waandishi wa habari zinazohusu mchakato wa mabadiliko ya sheria za habari nchini.

Jukwaa hilo limefanya kikao na wanataaluma washauri (mentors) wa waandishi hao juzi jijini Dar es Salaaam, kwa lengo la kuweka mikakati ili kufikia malengo ya kufanya mabadiliko ya sheria za habari.

Mwenyekiti wa TEF, Deodatus Balile, alisema lengo la uteuzi wa timu hiyo unalenga kuongeza chachu ya harakati kuelekea mabadiliko Sheria za Habari nchini.

"Tunapaswa kuwa na waandishi wabobezi katika harakati hizi, ndiyo maana tumeunda timu ya wanataaluma ambao watawasimamia waandishi ili waweze kupita njia itakayoleta mafanikio.

"Mimi kama mwenyekiti naamini, timu hii ya wataalamu wabobezi, itasaidia kwa kiwango kikubwa kunyoosha mwelekeo na hatimaye kupata matokeo chanya," alisema Balile.

Wanataaluma walioteuliwa kusimamia waandishi hao ni Joseph Kulangwa, Mhariri wa Raia Mwema; Stella Aron, Mhariri wa Majira; Rashidi Kejo, Mhariri wa Mwananchi; Angela Mangenya, Mhariri wa TBC na Joseph Nakajumo na Wahariri Wastaafu.

# Wafanyabiashara waiangukia serikali kushusha gharama gesi

**Na Beatrice Shayo**

BAADHI ya wafanyabiashara wameiomba serikali kushusha gharama za gesi ili kuondokana na matumizi ya kuni na mkaa ambayo yanasababisha uharibifu wa mazingira na madhara kwa afya.

Akizungumza na gazeti hili kiongozi wa wakaanga samaki soko la feri, Ally Mbonde, alisema gharama za kutumia gesi ni kubwa na zinawaumiza katika utendaji wao.

Alisema waliacha kutumia kuni na mkaa na kuanza kutumia gesi, lakini ujazo wake pia unaonekana kuchakachuliwa kutokana na hapo awali mtungi wa kilo 36 unaouzwa kwa Sh. 95,000 ulitumika kwa siku tatu lakini sasa unatumika kwa siku moja.

"Sijui siku hizi wameufanya nini tunatumia siku moja matumizi ni yale yale, ndiyo changamoto yetu kubwa kwa wakaangaji wa samaki hii nishati ya gesi inatuumiza kwenye gharama."

"Afya zetu zimekuwa nzuri hata utendaji wetu wa kazi kwa sasa umeimarika uchafuzi wa mazingira hakuna kikubwa ni gharama inatuumiza serikali itutizame katika hilo bila kuwa na Sh. 200,000 kwa siku huwezi kufanya biashara, mtungi Sh. 95,000 na mafuta ya kupika dumu ni Sh 105,000," alilalamika.

Kabla ya kuingia katika nishati ya gesi, alisema walikuwa wananunua kuni hadi za Sh. 30,000 kwa siku kulingana na mzigo wa samaki uliopo ingawa afya zao zilikuwa hatarini.

Alisema pamoja na Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC), kuwaahidi kuwafungia mtungi wa pamoja, ahadi hiyo haijatekelezwa mpaka sasa.

Mamalishe anayetumia nishati ya kuni, Khadija Ismail, alisema wanashindwa kutumia gesi kutokana na hali zao za kipato kuwa za chini.

"Gesi ni nzuri haina moshi unaweza kuokoa mafuta kwa sisi wafanyabiashara wadogo wadogo kwa sababu unaivisha kwa haraka hali zetu za kipato zinatufanya tuendelee kutumia kuni," alisema.

Alisema matumizi ya kuni yanawaumiza kifua kwa sababu ya moshi na afya kuwa hatarini licha ya kuwa bei nafuu.

Alisema kuni tatu wananunua kwa Sh. 3,000 na usafiri gharama inafika Sh. 4,000 kutokana na ugumu wa maisha anaona bora kuegemea kwenye nishati hiyo ina changamoto.

Alisema serikali iangalie namna ya kufanya ili kupunguza gharama za gesi ili waweze kutumia nishati hiyo na kuondokana na matumizi ya kuni ambayo itasaidia kuepusha uharibifu wa mazingira.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Ndani kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), Elisha Osati, alisema madhara yanayotokana na kuni za kupikia yanaweza kuleta matatizo katika mapafu, kusababisha kutengeneza makovu ambayo yanaweza kumsababishia mtu kushindwa kupumua vizuri na wakati mwingine kupata kikohozi cha mara kwa mara.

"Ile mirija midogo midogo ambayo inapitisha hewa kwenye mapafu inatanuka inashindwa kufanya kazi yake vizuri inasababisha matatizo kwenye mapafu kushindwa kuweka hewa ya kutosha na kumsababisha mtu kupata magojwa ya maambukizi kwenye mapafu," alisema Dk. Osati.

Dk. Osati alisema moshi wa kuni una madhara hata wanaotumia mkaa kwa wingi wakati mwingine madhara ya mwili kukosa oksijeni ya kutosha na athari katika mapafu.

Alisema cha muhimu kuangalia ni namna bora ya wananchi kupata nishati mbadala ya kupikia ili wasipate madhara katika afya zao.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wachezaji tambueni nafasi zenu

**KLABU** za Ligi Kuu Tanzania Bara zipo kwenye maandalizi ya Ligi Kuu na usajili wa wachezaji kwa ajili ya msimu mpya wa Ligi Kuu.

Kanuni ya 33(1) ya Ligi Kuu Tanzania Bara inasema: "Mwalimu Mkuu wa timu atawajibika kutambua wachezaji wanaotakiwa kusajiliwa. Katibu Mkuu atafanya masuala ya utawala, atakamilisha shughuli ya usajili wa wachezaji na kuwasilisha mikataba na fomu ya majina TFF kwa wakati."

Nini sababu au madhumuni ya kanuni hiyo? Kwa kifupi kanuni hiyo inaainisha majukumu ya kocha (mwalimu) kama mtaalamu wa mpira wa miguu katika timu na Katibu (mtawala) kama mtaalamu wa uongozi katika klabu.

Kwa mujibu wa kanuni ya 33(3), walimu (makocha) wa klabu wanawajibika kutangaza majina ya wachezaji wanaoachwa, wanaositisha mikataba, uhamisho na usajili wa wachezaji katika kipindi kitakachotangazwa na TFF.

Usajili unafanywa ili kuziba nafasi ambayo iko wazi au kuimarisha timu kwa lengo la kufanya vizuri. Unapotaka kuimarisha timu ni lazima uwe na nafasi ambayo inaweza kutengenezwa kwa kuuza mchezaji, kuvunja mkataba wake au kutakiwa mahali kwa mkopo.

Kimsingi usajili una sura mbili tu. Kocha na mchezaji. Ni kocha kama mtaalamu wa mpira wa miguu kwa niaba ya klabu anayepanga au kuamua ni mchezaji wa aina gani anatakiwa kusajiliwa na kwa lengo lipi.

Tanzania kama zilivyo nchi nyingi za Afrika zina wachezaji wenye uwezo na vipaji. Lakini kuwa na kipaji kwa mchezaji ni kitu kingine kama ilivyo kwa mchezaji mwenye uwezo.

Hili ni eneo ambalo lina matatizo makubwa kwa wachezaji wa Tanzania. Kwa lugha yenye kueleweka ni kuwa kuna wachezaji wenye vipaji na uwezo mkubwa wa kucheza mpira wa miguu lakini bado hawajatambua nafasi zao.

Kutojitambua ni pamoja na mchezaji kutojua ni kwa nini anakwenda klabu X badala ya klabu Y. Nini mustakabali wake katika mpira wa miguu ambayo ni ajira isiyo na kiinua mgongo, lakini ni mchezo ambao umri ni moja ya vigezo vya msingi.

Katika uga wa mpira wa miguu Tanzania ni jambo la kawaida kwa mchezaji anayeng'ara kwenye klabu Y kuamua kwenda klabu X kwa vile tu ameonyeshwa fedha.

Ni kweli kila mtu anahitaji fedha katika maisha yake ikiwamo kutatua matatizo mbalimbali yanayomzunguka. Fedha katika hali ya kawaida ni kila kitu, kwani inaweza kuhamisha hata mlima. Lakini fedha hiyo inaichukua kwa utaratibu gani?

Ni kawaida mchezaji anayecheza katika kikosi cha kwanza katika klabu X kwenda klabu Y huku akijua dhahiri hawezi kupata nafasi katika kikosi cha kwanza.

Kwa mchezaji mwenye uwezo wa kucheza mpira wa miguu uamuzi wa aina hiyo ni wa kujimaliza.

Inaweza kuwa ni matatizo ya fedha yanamsukuma mchezaji kufanya uamuzi wa aina hiyo. Lakini kama kweli ni matatizo kwa nini aingie mkataba wa muda mrefu? Pata fedha, lakini uvumilie kukaa kwenye benchi kwa msimu mmoja tu.


Wapo wachezaji wenye uwezo wa kucheza mpira wa miguu, lakini hawaonekani kwa vile tu wameamua kukaa kwenye klabu Y wakati hawana nafasi katika kikosi cha kwanza cha klabu hiyo.

Unaweza kukaa misimu minne ukiwa benchi kwenye timu moja wakati una uwezo wa kucheza mpira wa miguu katika klabu za Ligi Kuu zilizobaki.

Hiki ni kipindi cha usajili. Lakini ni kipindi ambacho wachezaji wenye uwezo na vipaji wanatakiwa kufanya uamuzi mgumu kwa lengo la kulinda uwezo na vipaji vyao, vinginevyo watasahaulika katika medani hii ya mpira wa miguu.

Fursa ya kuchezea Timu ya Taifa (Taifa Stars) iko wazi kwa mchezaji yeyote mwenye uwezo, na anayecheza katika kikosi cha kwanza katika klabu yake. Hakuna kocha anayeingiza mchezaji kwenye Timu ya Taifa wakati hana nafasi hata katika klabu yake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Vitumike viwanja vichache, vingine visipoboreshwa

Na Adam Fungamwango

**KABLA** hata ya kuanza kwa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2022/23 hapo Agosti 17, Bodi ya Ligi Kuu Tanzania Bara imevipiga 'stop' viwanja saba vilivyokuwa vinatumika kwenye ligi msimu uliopita hadi hapo vitakapofanyiwa marekebisho.

Viwanja hivyo ni Mkwakwani Tanga, Ilulu Lindi, Ushirika Kilimanjaro, Mabatini Pwani, Sokoine Mbeya, Jamhuri Dodoma na Nyankumbu Girls, Geita.

Kwenye taarifa yao inasema, pamoja na kwamba wanasubiri taarifa ya ukaguzi wa viwanja unaofanywa na Kamati ya Leseni za Klabu iliyo chini ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), lakini imefanya tathmini ya viwanja vilivyotumika kwenye mechi za Ligi Kuu msimu uliomalizika na kubaini mapungufu kadhaa kwenye viwanja hivyo.

Baada ya kuainisha mapungufu hayo, binafsi naiunga mkono Bodi ya Ligi kwa sababu kama ikileta huruma kwenye hili, basi Tanzania itakuwa inacheza Ligi Kuu yake kama vile bonanza, michuano ambayo haifuati sheria wala kanuni yoyote ile.

Pia kama itafumbia macho suala hili, hakuna nguvu yoyote itakayotumika ili kuvikarabati na hata viwanja ambavyo kwa sasa ni vizuri, basi wamiliki wao hawatofanya mkazo kuendelea kuvifanya kuwa bora kwa kuona na wao wataonewa huruma.

Mapungufu 10 ambayo Bodi ya Ligi imeyabainisha ni mengi sana, tena mengine yana vipengele vyake.

Namba moja ni eneo la kuchezea kutokuwa tambarare na kukosa nyasi za kutosha, pili ni ubovu katika uzio wa kutenganisha mashabiki na eneo la kuchezea, tatu jukwaa kuu kukosa ubora, ikiwamo ubovu wa paa.

Nne ni vyumba vya kuvalia nguo za wachezaji na waamuzi kukosa sifa nne ambazo zimeainishwa pia.

Nao ni ukubwa stahili pamoja na feni, AC kwa ajili ya upatikanaji wa hewa ya kutosha, upatikanaji wa majisafi na ya kutosha muda wote, upatikanaji umeme na uwepo wa vyoo safi na vya kisasa.

Kukosekana kwa mabenchi ya ufundi bora na yenye uwezo wa kuruhusu watu wasiopungua 17 kuketi.

Namba tisa ni kukosekana kwa majukwaa kwa ajili ya watazamaji na 10 ni uwepo na mabango, picha za matangazo zisizotambulika na TFF na Bodi ya Ligi.

Ukiangalia mapungufu haya utaona kuwa kuna mapungufu makubwa na matatizo kwenye soka la Tanzania kwa upande wa miundombinu.

Wakati klabu zikisonga mbele kwa kuwekeza na kusajili wachezaji wa gharama za juu, huku waandishi na mashabiki mbalimbali wa soka Afrika wakianza sasa kulifuatilia soka la Tanzania kutokana na kukusanya wachezaji toka kila pande ya Afrika, viwanja vyetu bado vinatushusha thamani.

Wadhamini mbalimbali, wakiwamo wa televisheni ambao wanaonyesha michezo hiyo wamekuwa wakilihеshimisha soka la Tanzania kwa kuonyesha mechi nyingi, lakini wakati mwingine inakuwa aibu kuonyesha mechi ambazo uwanja hauna nyasi, umechimbika, au maji yametuama mechi inachezwa na matope uwanjani.

Bodi ya Ligi imezitaka klabu zinazotaraji kutumia viwanja hivyo kufanya jitihada za makusudi katika kuboresha maeneo yalioainishwa ili kukidhi matakwa ya kanuni na sheria zinazoongoza mpira wa miguu.

Hii ni kwamba kama haitokuwa hivyo, basi itabidi zihame kwa kuchagua viwanja mbadala.

Cha kufanya hapa ni kwamba klabu zishirikiane na wamiliki wa viwanja ili kukarabati sehemu ambazo kwao zina changamoto ili viruhusiwe.

Kwa hali hii ni afadhali hata ligi ikachezwa kwenye viwanja vichache kuliko viwanja vibovu ambavyo vinaharibu ladha ya soka, mifumo wa makocha, ubora na ufundi wa wachezaji miguuni pamoja na ligi yenyewe.

Ni bora ligi iwe inachezwa kila siku, mchana na usiku kwenye viwanja vichache vyenye ubora kama Benjamin Mkapa, Azam Complex, CCM Kirumba, Nyamagana na Kaitaba kuliko ligi ya Tanzania ambayo kwa sasa imekuwa na hadhi kubwa Afrika kuchezwa kwenye viwanja visivyokidhi viwango.

Tunajua kuwa serikali imesema itavitengeneza baadhi ya viwanja, hiyo ni baadaye, lakini kwa muda huu ambao msimu wa Ligi Kuu 2022/23 unataka kuanza ni lazima timu zinazotaka kutumia viwanja hivyo kushirikiana na wamiliki wa viwanja kwa ajili ya kuweka mambo sawa.

**TOLEO MAALUM**

# TANESCO YANYAKUA TUZO YA SEKTA YA MADINI MAONYESHO YA SABA SABA

**Na Renatha Msungu**

JULAI saba kila mwaka, Tanzania inaazimisha maonyesho ya kimataifa ya biashara, maarufu kama 'Saba Saba' ambayo hufanyika Jijini Dar es Salaam kwa lengo la kuchochea ufanisi na ubora wa sekta hiyo muhimu kwa maendeleo ya uchumi wa nchi.

Kwa mwaka huu (2022) maonyesho hayo yaliyofikia kilele chake Julai 13, kwa kushuhudia baadhi ya Taasisi, Kampuni na Mashirika yakipata tuzo mbalimbali kutokana na ufanisi mzuri.

Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) ni miongoni mwa mashirika yaliyoshiriki katika maonyesho hayo na kufanikiwa kutunukiwa tuzo na heshima kutokana na utendaji kazi mzuri unaofanywa kila iitwapo leo na shirika hilo.

TANESCO, iliibuka mshindi wa kwanza katika sekta ya nishati na kutunukiwa tuzo hiyo na Makamu wa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania,Dk Philiph Mpango, aliyekuwa mgeni rasmi kwenye sherehe ya kufunga maonyesho hayo iliyofanyika Julai 13, 2020.

Tuzo hiyo na tuzo nyingine ambazo shirika hilo liliwahi kupata katika maonyesho mengine ya kibiashara, imekuwa chachu ya TANESCO kuendelea kufanya vizuri zaidi katika utendaji wao,ikiwemo kuzidi kufanya maboresho mbalimbali ili kuhakikisha shirika hilo linapiga hatua katika kazi inazozifanya za utoaji huduma za umeme kwa wateja wake pamoja na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya Taifa.

Akizungumza na Nipashe mara baada ya kukabidhiwa tuzo hiyo,Msemaji wa TANESCO Martin Mwambene amesema ushindi huo unaashiria mabadiliko,Mapinduzi ikiwemo maboresho mbalimbali yanayoendelea kufanyika katika Shirika hilo kuanzia kwenye uzalishaji ,usafirishaji,usambazaji wa umeme na utoaji huduma mbalimbali za shirika hilo kwa jamii.

Mwambene anafafanua kuwa,Shirika limeweza kufanya hayo kutokana na juhudi kubwa katika kuwaelimisha vizuri wananchi na wageni mbalimbali waliotembelea ili kujionea shughuli zinazofanywa na TANESCO, kitendo kilichochangia kuongeza uwelewa kwa jamii na taifa kwa ujumla.

"Tumekuwa tukijibu vizuri maswali mbalimbali ya wananchi na wateja waliotembelea kwenye banda wakati wa maonyesho lakini pia, kwa wale wanaopiga simu ili kupata ufafanuzi kuhusiana na mambo mbalimbali yanayohusu shirika hilo,"amesema Mwambene.

Amesema pia, ukiacha hayo, wakati wa maonyesho hayo waliwaonyesha wananchi waliojitokeza katika Banda hilo utekelezaji wa mradi mkubwa na wakimkakati wa kuzalisha umeme wa Mwalimu Julius Nyerere ambao unaendelea vizuri na kwa sasa umefikia asilimia 63.

"Mradi huu umekuwa kivutio kikubwa sana kwa wananchi waliojitokeza katika maonyesho na walipata maelezo mazuri juu ya namna unavyotekelezwa,"amesema Mwambene.

"Wateja wengi wamekuwa wakijitokeza katika eneo hilo ili kufahamu nini kinaendelea katika mradi huo na shirika limeweza kuwapa maelezo kwa kutumia picha na video ili kuwaonyesha namna utekelezaji na umuhimu wa mradi huu,"amesema.

Ukiacha hayo,Mwambene amesema wamefanikiwa pia kuwaonyesha namna ya mfumo wa gridi ya Taifa unavyoendeshwa sambamba na miundombinu ambayo ipo kwenye gridi hiyo ikiwemo kuonyesha juhudi za shirika za kuunganisha nchi nzima na gridi ya Taifa.

Amefafanua kuwa wananchi mbalimbali ambao walijitokeza katika maonyesho hayo wamefanikiwa kuona miradi tarajiwa ya shirika hilo inayokwenda kutekelezwa ikiwemo Kigoma,Sumbawanga na Rukwa mikoa ambayo mpaka sasa haijaingia kwenye gridi ya Taifa.

"Shirika lina kila sababu ya kujivunia kutokana na kupata tuzo hiyo na uhakika na utendaji tunaofanya na kuongeza wananchi watarajie makubwa siku zijazo,"amesema Mwambene.

Mbali na hayo,pia Mwambene amesema waliwaonyesha wananchi miradi ya vituo vya kupooza na kusambaza umeme ikiwemo jinsi inavyofanya kazi kupitia video.

Hata hivyo anasema wateja wengi wameweza kujionea huduma ya Nikonekt ambayo imeleta mapinduzi makubwa katika huduma za kuunganisha umeme pasipo kufika kwenye ofisi za shirika,ambapo huduma hiyo imeonekana kuwafurahisha wananchi kwa sababu haina usumbufu wowote.

"Hii huduma ilikuwa kivutio kwa wateja,wengi wao walisema inasaidia kuepusha msongamano kwa wale wanaohitaji kuunganishiwa umeme,"amesema Mwambene.

Amesema sehemu hii pia ilivutia sana wananchi wengi ambao walifika kwenye banda la Tanesco kwa ajili ya kujionea shughuli mbalimbali zinazofanywa na shirika hilo.

Anasema pia wananchi wameshuhudia shughuli zinazofanywa na Shirika la Maendeleo ya Jotoardhi (TGDC) ambayo ni kampuni tanzu ya TANESCO ambao wao walionyesha wananchi namna umeme unavyozalishwa kwa kutumia jotoardhi.

"Hili nalo lilikuwa eneo muhimu sana kwa wateja na raia waliojitokeza katika maonyesho hayo ambayo yalifunguliwa rasmi Juni 28 na kufikia kilele chake Julai 13 kwa Makamu wa Rais kufunga"aliongeza.




*Waziri wa nishati mhe. January Makamba alipata maelezo kutoka kwa Gilbert Minja kutoka kampuni ya Motion Africa kuhusu gari inayotumia umeme (Electric Vehicle) alipotembelea maonyesho ya Sabasaba*




*Kaimu meneja uhusiano na mawasiliano wa shirika la umeme nchini Irene Marobe (Kushoto) akimkabidhi zawadi ya mkoba wenye nembo ya Nikonekt Katibu wa Itikadi na Uenezi wa Chama cha Mapinduzi Ndg. Shaka Hamdu Shaka wakati alipotembelea banda la shirika hilo.*



*Baadhi ya wananchi waliyotembelea banda la TANESCO wakipata maelezo kutoka kwa Patrick Mwakyoma kutoka shirika la umeme nchini juu ya mradi wa kufua umem kwa njia ya maji wa bwawa la Julius Nyerere.*



*Maafisa kutoka shirika la umeme nchini Tanesco wakimsikiliza mteja aliyefika katika bandaa la TANESCO katika maonesho ya Sabasaba*

tanesco_official_page umemeforum.blogspot.com tanescoyetultd tanescoyetu

216947701

# Wanafunzi wawili wafariki dunia kwa kufukiwa na kifusi

**Na Gideon Mwakanosya,**
SONGEA

WANAFUNZi wawili wa Shule ya Lupapila, Halmashauri ya Manispaa ya Songea, mkoani Ruvuma, wamefariki dunia baada ya kufukiwa na kifusi wakati wakichimba mchanga kandokando ya Mto Ruvuma.

Habari zilizopatikana jana mjini hapo na kuthibitishwa na Ofisa Mtendaji wa Kata ya Subira, Alexander Kapinga, zinasema tukio hilo lilitokea Julai 14, mwaka huu, majira ya saa 12 jioni. Aliwataja waliofariki dunia kuwa ni Idelphonce Mwageni, mwanafunzi wa darasa la saba na Musa Chabruma wa darasa la tano.

Alisema siku ya tukio, wanafunzi watatu baada ya kumaliza masomo walikwenda kando ya Mto Ruvuma kwa ajili ya kuchimba mchanga kwa lengo la kujipatia kipato.

Alidai wakati wakiwa wanachimba mchanga huo, kifusi kiliwafunika huku mmoja ambaye jina lake halikupatika akinusurika kwa kuwa alikuwa nje ya shimo. Alisema manusura huyo alitoa taarifa kwa majirani ambao waliwajulisha viongozi wa serikali ya mtaa na baadaye vyombo vya dola ambao waliwapoa kutoka kwenye kifusi hicho wakiwa hai na kuwapeleka hospitalini, lakini walifariki muda mchache wakati wakipatiwa matibabu.

Akizungumzia tukio hilo, Ofisa Elimu Msingi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea, Frank Sichalwe, alithibitisha kutokea kwa vifo hivyo.

Diwani wa Kata ya Subira, John Ngonyani alisema ilikuwa kawaida kwa wanafunzi hao kuchimba mchanga ili kujipatia kipato kila baada ya masomo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Joseph Konyo, alithibitisha kutokea kwa vifo vya wanafunzi hao.




Baadhi ya wafanyabiashara wakifuatilia kwa makini mada mbalimbali zilizotolewa katika hafla ya ufunguzi wa NMB Business Klabu iliyofanyika ukumbi wa Sea View Beach Resort Manispaa ya Lindi mkoani Lindi. Benki ya NMB iliwafunda zaidi ya wafanyabiashara 700 kutoka mikoa ya Mtwara, Lindi na Mbinga kuhusu elimu ya biashara na fedha. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Majaliwa aiagiza TARURA kumwengua mkandarasi

**Na Thobias Mwanakatwe,**
MANYONI

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameagiza Wakala wa Barabara Mjini na Vijijini (TARURA) Mkoa wa Singida kuvunja mkataba na mkandarasi wa Kampuni ya Bullem Investment Limited, iliyopewa kazi ya kujenga barabara mjini Manyoni kwa gharama ya Sh. milioni 495.

Kampuni hiyo ilipewa zabuni kujenga barabara kutoka kitongoji cha Majengo hadi katika Hospitali ya Wilaya ya Manyoni, imeshindwa kukamilisha kazi hiyo kwa wakati.

Alitoa agizo hilo juzi wilayani Manyoni baada ya kupata malalamiko ya wananchi ambao walizuia msafara wake na kumweleza kuwa ujenzi wa barabara hiyo umechukua muda mrefu kukamilika na kusababisha usumbufu kwa wakazi wa eneo hilo.

"Kama mkandarasi ni msumbufu mwondoe, kapitie mkataba wake urekebishe kuokoa kuendelea na mkandarasi mzembe," alisisitiza Majaliwa wakati akimwagiza Meneja wa TARURA Mkoa wa Singida, Mhandisi Tembo David.

Pia aliigiza TARURA kukagua na kumlipa mkandarasi huyo kulingana na asilimia zilizofikiwa katika ujenzi wa barabara hiyo na asilimia zilizobaki apatiwe makandarasi mwingine atakayeweza kukamilisha kazi hiyo kwa wakati.

Awali, Meneja wa TARURA mkoa, alimweleza Waziri Mkuu moja ya sababu za kuchelewa kukamilika kwa wakati mradi kuwa ni uzembe wa mkandarasi huyo.

Alisema tayari ameshalipwa Sh. milioni 95 kati ya Sh. milioni 495 anazotakiwa kulipwa na hadi sasa ameijenga barabara hiyo kwa kiwango cha asilimia 50 na ilikuwa akamilishe ujenzi Juni, mwaka huu.

## CRDB yawafunda wafanyabiashara mtandaoni

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuendeleza jitihada zake za kuwajengea uwezo na kuwawezesha wajasiriamali vijana nchini, Benki ya CRDB imeandaa semina maalum iliyopewa jina la 'CRDB Bank Instaprenyua', ili kuwawezesha vijana ambao wanafanyabiashara kupitia mitandao ya kijamii.

Semina hiyo ilifanyika juzi Makao Makuu ya Benki hiyo, jijini Dar es Salaam.

Akizungumza wakati akifungua semina hiyo, Ofisa Mkuu wa Biashara wa Benki ya CRDB, Boma Raballa, alisema katika miaka ya karibuni kumekuwa na mwamko mkubwa kwa vijana kujishughulisha na shughuli za ujasiriamali, hususani kupitia mitandao ya kijamii ambayo imerahisisha namna ya kuendesha biashara na kuyafikia masoko kwa urahisi.

"Vijana wamekuwa wakitumia vizuri fursa zilizoko hususani za mitandao ya kijamii kufanikisha shughuli zao za ujasiriamali. Tumewaona vijana wajasiriamali ambao wanafanya vizuri kupitia maduka mtandao, jambo ambalo limetusukuma kuwapa elimu na kuwajengea uwezo," alisema Raballa.

Alisisitiza kuwa biashara mtandao ni moja ya eneo linalokua kwa kasi na linalopaswa kuangaliwa, ikiwa ni pamoja na kutafuta suluhu ya kuwawezesha wajasiriamali hao.

Pia mitandao ya kijamii, hususan Instagram, Facebook na Twitter, imekuwa chachu kubwa kwa vijana wajasiriamali nchini kuishi ndoto zao za ujasiriamali.

"Takwimu zinaonyesha Instagram ndiyo mtandao wa kijamii wenye watumiaji wengi zaidi duniani, bilioni 1.074. Vivyo hivyo hapa Tanzania, mtandao huo unaongoza pia kwa wafuasi zaidi ya milioni 2.86.

"Hii ndiyo sababu ya kuipa jina la Instaprenyua semina hii kwani ndipo hasa vijana wengi wapo, lakini lengo ni kuwafikia vijana katika majukwaa yote ya mtandaoni," alisema.

Akizungumzia malengo ya kuandaa semina hiyo, Mkuu wa Kitengo cha Masoko wa Benki ya CRDB, Joseline Kamuhanda, alisema semina hiyo ina malengo makuu matano ambayo ni pamoja na kutoa mafunzo ya namna bora ya kuendesha biashara kwa wajasiriamali wanaofanya biashara mtandao, na kutoa elimu ya usimamizi wa fedha katika biashara.

Malengo mengine kwa mujibu wa ofisa huyo ni kutoa elimu ya masoko ya fedha na mitaji, na namna bora za kuyaendea masoko hayo, elimu juu ya fursa zinazotolewa na Benki ya CRDB kwa wajasiriamali nchini, pamoja na elimu ya urasimishaji wa biashara na faida zake kwa wajasiriamali.

# Zaidi ya wananchi 90,000 kuchanja UVIKO-19

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WANANCHI 93,729 mkoani Njombe wanatarajiwa kufikiwa na kampeni ya utoaji chanjo ya Uviko-19 awamu ya tatu, itakayotolewa mtaa kwa mtaa kwa ajili ya kuongeza idadi ya waliochanja katika kukabiliana na ugonjwa huo.

Taarifa hiyo ilitolewa na Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Waziri Kindamba, wakati akizungumza na waandishi wa habari mkoani hapo kuhusu utoaji wa chanjo hiyo ya Uviko -19, ulioanza Julai 11 na kukamilika Julai 18, mwaka huu.

Alisema serikali mkoani humo imejipanga kutoa huduma hiyo kwa wataalamu wa afya kupita mtaani na kwenye mikutano ya hadhara inayofanywa na viongozi wa serikali ili kuwafikia watu wengi zaidi.

Kwa mujibu wa Kindamba, kampeni hiyo imeonesha mafanikio kwa kuwa mpaka sasa kiwango cha watu kujitokeza kuchanja kimeongezeka mara mbili ikilinganishwa na awali.

Aidha, alisema ni muhimu wananchi wakafahamu kuwa magonjwa ya mlipuko yana tabia ya kujirudia na huja kwa nguvu zaidi kwa kuwa kirusi kinajibadilisha zaidi, na kwamba tahadhari isipochukuliwa madhara ni makubwa.

"Takwimu zetu za hapo nyuma zilikuwa hafifu sana na kama mnavyoona wakuu wa wilaya wanazunguka huko wanahamasisha, magari yanapita yanahamasisha tunatumia mpaka wasanii lengo letu wananchi wa Njombe wahamasike na wawe na mwamko zaidi wa kuchanja kuliko hapo nyuma," alisema Kindamba.

Awali, Mratibu wa Chanjo Mkoa wa Njombe, Linda Chatila, aliwataka wananchi kuondokana na imani potofu zinazowafanya watu wengi kusita kuchanja, huku akitaja za dini na nyingine kuamini chanjo ina madhara.

Alisema chanjo UVIKO-19 kwa awamu ya tatu itaenda mbali zaidi kwa kutolewa nyumba kwa nyumba na katika mikusanyiko mbalimbali ili wananchi wengi zaidi waweze kupata chanjo hiyo.

Tangu kuanza kwa huduma hiyo, siku ya kwanza walichanja watu asilimia 52 ya lengo kwa waliojitokeza na iliongezeka hadi asilimia 81.

## Wakumbushwa kuzingatia matibabu ya paka, mbwa

**Na Julieth Mkireri,** CHALINZE

WATANZANIA wametakiwa kuzingatia matibabu ya mara kwa mara ya paka na mbwa wanaofugwa kujilinda na magonjwa yanayosababishwa na wanyama hao.

Dk. Obeid Kiariro, kutoka Chalinze alikuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu usambazaji wa dawa za mifugo kutoka Kampuni ya Tansoko Agrovet ambayo imeshiriki kwenye maonyesho ya ufugaji kibiashara yaliyofanyika Ubena.

Alisema suala la afya ya wanyama linatakiwa kupewa kipaumbele kwa kuwa kuna magonjwa ambayo yasipotibiwa mapema yanaweza kuwaathiri wanadamu.

"Watanzania bado hawajatoa kipaumbele matibabu ya wanyama hususani paka na mbwa, lakini hawana elimu ya kutosha kuwa baadhi ya magonjwa wanayopata mengine yanachangiwa na wanyama hao," alisema.

Alisema Tansoko Agrovet kwa sasa wanaendelea na usambazaji wa dawa hizo za mifugo katika maeneo mbalimbali nchini ili kuwezesha dawa hizo kuwafikia wafugaji kwa wa ukaribu.

Akizungumza kwenye maonyesho hayo yaliyoandaliwa na Chama cha Wafugaji wa Ng'ombe kibiashara (TCCS), Mshauri mwelekezi, Dk. Peter Makang'a, kutoka Baraza la Nafaka la Serikali ya Marekani, alisema Baraza hilo kwa sasa linatarajia kuanza kutoa mafunzo kwa wafugaji wa mifugo.

Alisema Baraza hilo ambalo linafanya kazi katika nchi 42 duniani baada ya kuwekeza kwa muda mrefu kwenye ufugaji wa kuku sasa linatarajia kuanza upande wa mifugo hususani ng'ombe.




Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi wa Benki ya Stanbic, Omari Mtiga (kushoto), akikabidhi moja ya madawati 50 yaliotolewa na benki hiyo kwa Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Heri James (katikati) na Mkuu wa Shule ya Sekondari Kimara, Elizabeth Bonzo (kulia). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Stanbic yaahidi kuboresha mazingira shule za serikali

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Stanbic Tanzania imesisitiza ahadi yake ya kuendelea kuunga mkono juhudi za serikali za kuboresha elimu kwa kuweka vizuri mazingira ya kujifunzia shule za serikali.

Benki hiyo ilitoa ahadi hiyo wakati wa hafla fupi iliyofanyika katika Shule ya Sekondari Kimara ya kukabidhi madawati 50 yenye thamani ya Sh. 4,500,000 waliyo yakabidhi kwa taasisi hiyo ya elimu.

Msaada huo ni sehemu ya kampeni inayoendelea ya benki hiyo 'Stanbic Madawati Initiative', inayolenga kupunguza uhaba wa madawati shuleni kwa kuchangia nchi nzima na kupanda mti mmoja kwa kila dawati linalotolewa ili kuhakikisha uwiano katika mfumo wa ikolojia wa mazingira.

Madawati hayo yalikabidhiwa na Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi wa Benki ya Stanbic, Omari Mtiga kwa Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Heri James, katika hafla iliyofanyika shuleni hapo mwishoni mwa wiki.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo Mtiga alisema: "Tunatambua juhudi zinazofanywa na serikali katika kuboresha sekta ya elimu, na tumejipanga kuwa mstari wa mbele kuunga mkono juhudi hizo kwani tunaamini kuwa elimu bora ni muhimu katika kujenga jamii yenye watu wenye uelewa mpana, ambao ni chachu ya maendeleo ya sekta mbalimbali za uchumi wa taifa."

Pia dhumuni la benki hiyo kuendelea kujitolea kusaidia sekta ya elimu ni kusukuma gurudumu la maendeleo ya nchi kwa kuunga mkono ndoto za jamii ndani ya maeneo inayofanyia kazi.

"Kupata nafasi ya kuchangia maendeleo ya elimu nchini Tanzania ni heshima kwetu kwani tunawawezesha wanafunzi kutimiza ndoto zao na kuchochea kufikia dira ya taifa ya kuleta maendeleo kwa kila Mtanzania," alisema Mtiga.

Akizungumza katika hafla hiyo, James alisema kuwa mchango wa Benki ya Stanbic ni kielelezo kuwa juhudi za serikali kuweka mazingira rafiki kwa taasisi za fedha na taasisi nyingine kufanya biashara zinazaa matunda, hivyo kuziwezesha taasisi hizo kuwekeza katika jamii.

Alisema pamoja na juhudi zake zote, serikali haiwezi kuendeleza sekta zote kwa wakati mmoja kwa asilimia 100 kwa sababu fedha za taifa zinagawanywa kwa sekta zote kulingana na mahitaji. Aliwataka wadau kuunga mkono juhudi za serikali ili kukidhi mahitaji ya wananchi.

"Serikali yetu imewekeza katika ujenzi wa madarasa, hata hivyo, kuna uhaba wa madawati, mchango wa Stanbic wa madawati haya leo unaunga mkono juhudi za serikali za kuboresha mazingira ya elimu katika shule hii, kuwezesha watoto kufikia ndoto zao," alisisitiza.

# Simbachawene: Kampeni ya GGM imesaidia mapambano ya UKIMWI

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu-Sera, Bunge na Uratibu, George Simbachawene, amesema jitihada za Kampeni ya GGM Kili Challenge pamoja na wadau mbalimbali kwa kushirikiana na serikali, zimesaidia kupunguza vifo vitokanavyo na VVU/Ukimwi kwa asilimia 50 kutoka vifo 64,000 mwaka 2010 hadi 32,000 mwaka 2020.

Pia maambukizi mapya ya VVU kwa watu wazima (miaka 15 na zaidi), yameshuka kutoka 110,000 mwaka 2010 hadi 68,000 mwaka 2020, wakati maambukizi mapya kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto yameshuka kutoka asilimia 18 mwaka 2010 hadi asilimia saba mwaka 2020.

Simbachawene alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki wakati akiwaaga wapanda Mlima Kilimanjaro 52 ambao kati yao 28 wanauzunguka mlima kwa baiskeli na 24 kwa kutembea kwa miguu.

Upandaji mlima huo ulianza Julai 15, 2022, ukiratibiwa na Kampuni ya Geita Gold Mine Limited (GGML) kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS), kwa lengo la kuchangia fedha kwa ajili ya shughuli za udhibiti wa Ukimwi. Wapanda mlima hao watashuka Julai 21, mwaka huu.

Pamoja na mambo mengine, Simbachawene alisema serikali itaendelea kuwa mstari wa mbele kuhakikisha kuwa afua zinazotekelezwa za mwitikio wa VVU na UKIMWI zinaleta tija kwa makundi mbalimbali katika jamii.

Alisema ili kufikia malengo hayo pamoja na mengine katika kuishinda vita dhidi ya VVU na UKIMWI, kunahitaji nguvu ya pamoja kati ya serikali na wadau wengine, hususan sekta binafsi ili kupata rasilimali fedha ya kutosha.

"Kili challenge inalenga kupunguza athari za kupungua kwa misaada ya wahisani na kuiwezesha nchi kuimarisha uwezo wa ndani kwa ajili ya kudhibiti UKIMWI," alisema.

Makamu wa Rais wa AngloGold Ashanti - GGML anayesimamia miradi endelevu kwa upande wa Ghana na Tanzania, Simon Shayo, alisema kampeni hiyo imepiga hatua kubwa tangu kuanzishwa kwake mwaka 2002 hadi kufikia kuwa mfuko wa kimataifa, wenye kushirikisha wapanda mlima na waendesha baiskeli zaidi ya 700 kutoka mabara sita na zaidi ya nchi 20.

Alisema kupitia kampeni hiyo, taasisi mbalimbali zimenufaika kwa kupata fedha za kutekeleza shughuli za mwitikio wa VVU na Ukimwi nchini.

"Kwa mfano, mwaka 2020 Mfuko wa Kilimanjaro Challenge ulitoa fedha taslimu milioni 800 kwa taasisi 20 zisizo za kiserikali. Tunawakaribisha sana wadau wa kampuni mbalimbali kuchangia na kushiriki katika kampeni hii," alisema Shayo.

Aliishukuru Serikali ya Tanzania kwa msaada wake na ushirikiano wa TACAIDS katika kampeni ya Kili Challenge tangu kuanzishwa kwake mwaka 2002.

Mkurugenzi Mtendaji wa TACAIDS, Dk. Leonard Maboko, alisema kwa muda wa miaka 20 tangu kampeni hiyo ianzishwe zaidi ya Sh. bilioni 11, zimekusanywa na kusaidia katika kuendeleza mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI.

Alisema licha ya maendeleo mazuri yatokanayo na jitihada hizo, bado kuna maeneo ambayo yanahitajika nguvu zaidi ili kudhibiti ifikapo mwaka 2030 kama inavyoelekezwa katika malengo ya kidunia.

"Mojawapo ya malengo hayo ni kuzuia maambukizi mapya ya VVU hasa kwa vijana kwani zaidi ya theluthi moja ya maambukizi mapya hutokea kwa vijana wenye umri wa miaka 15-24, hususan wa kike," alisema.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, George Simbachawene (wa pili kushoto), akimkabidhi bendera mmoja wa washiriki wanaopanda Mlima Kilimanjaro kwa lengo la kukusanya fedha za mapambano dhidi ya VVU kupitia kampeni ya GGM Kili Challenge 2022. Kushoto ni Mkurugenzi wa TACAIDS, Dk. Leonard Maboko. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Baba wa kambo matatani udhalilishaji mtoto

**Na Joctan Ngelly, GEITA**

MKAZI wa Butundwe, Baiti Petro (26), amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Geita, kwa shtaka analodaiwa la kumsugulia uume wake mtoto mwenye umri wa miaka mitano.

Mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa mahakama hiyo, Cleofas Waane, Wakili wa Serikali, Shukran Msuya, alidai kuwa mtuhumiwa huyo alitenda kosa hilo nyumbani kwake.

Alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na kuomba tarehe nyingine ya kusomewa maelezo ya awali.

Hakimu alisema dhamana ya mtuhumiwa huyo iko wazi, kwa kutakiwa kuwa na wadhamini wawili wenye barua za utambulisho kutoka kwa Ofisa Mtendaji wa kata na mali isiyohamishika yenye thamani ya Shilingi milioni tatu kila mmoja.

Mtuhumiwa alishindwa kupata wadhamini na kuswekwa rumande mpaka kesi yake itakapopelekwa mahakamani Julai 28, mwaka huu, kusomewa maelezo ya awali.

# SBL yajipanga kudhibiti hewa ukaa

**Na Frank Monyo**

KAMPUNI ya Bia ya Serengeti (SBL), imesema inatekeleza mpango wa miaka 10 wa kupunguza na kumaliza utoaji gesi ya ukaa katika shughuli zake kufikia mwaka 2030, katika jitihada za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Nia yake hiyo ni kuendelea kuunga mkono jitihada mbalimbali zinazolenga kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Akiongea wakati ya kampeni ya kupanda miti hivi karibuni, Mkurugenzi Mtendaji wa SBL, Mark Ocitti, alisema kampuni hiyo inatambua umuhimu wa utunzaji wa mazingira kwa kuwa ni manufaa kwa watu wote.

"Kupitia kampuni yetu mama ya Diageo, SBL tunatekeleza mpango wa miaka 10 wa kupunguza na kumaliza kabisa utoaji gesi ya ukaa katika shughuli zetu kufikia mwaka 2030," alisema na kuongeza;

"Katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, SBL imekuwa ikijizatiti kukabiliana na ukataji miti kwa kupanda miti mingi nchini. Mwezi huu SBL imepanda miti takriban 5,000 mjini Dodoma. Juhudi hizi ni sambamba na rai iliyotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan kwa wakazi wote wa Dodoma kufanya makao makuu ya nchi kuwa ya kijani," alibainisha.

Kwa miaka miwili mfululizo, kampuni hiyo imeanza kupanda miti mwaka 2021 wilayani Kongwa na mwezi Julai ilikuwa Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe.

"SBL na kampuni yake mama Diageo, inaunga mkono jitihada za utunzaji wa mazingira kama kitovu cha mafanikio ya mchakato wa uzalishaji.

Upandaji miti huu Dodoma ni moja ya jitihada hizo zinazolenga kupanda mamilioni ya miti nchi nzima."

"Tumefanya jitihada hizi tangu mwaka 2018 ambapo tulipanda maelfu ya miti katika wilaya za Same na Moshi kuchangia juhudi za kuongeza ukubwa wa mimea katika eneo la Mlima Kilimanjaro."

Naye Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, aliishuruku SBL kwa kuunga mkono jitihada za upandaji miti na kuongeza kuwa miti ina nafasi ya kipekee kwa maisha ya watu na kusisitiza kuwa bila miti hakuna maisha.

Nipashe
Spotika



MCHEZAJI BORA WA KILA TAIFA KOMBE LA DUNIA UK. 12-13




UWANJA WA AT&T

# MIJI NA VIWANJA VYA KOMBE LA DUNIA 2026

**NEW YORK,** Marekani

MAANDALIZI ya Kombe la Dunia la 2026 yameongezeka kwa kufichuliwa miji 16 iliyobahatika kuwa mwenyeji.

Ikiwa imegawanywa kote Marekani, Canada na Mexico, Kombe la Dunia la 2026 ni la kwanza ambalo litashirikisha timu 48 na pia kuandaliwa na nchi tatu tofauti.

Hebu tuangalie viwanja 16 ambavyo michuano hiyo itafanyika.

***1. Atlanta - Mercedes-Benz***

Timu inayoutumia: Atlanta United

***Mashabiki: 75,000***

Kinachoanza ni Uwanja wa Mercedes-Benz huko Atlanta, ambao huwa mwenyeji wa mechi za Ligi Kuu ya Soka ya Marekani, MLS na NFL mara kwa mara.

Unatofautiana na paa lake la duara, ambalo huwa linauwezo wa kuondolewa na kurudishiwa.

***2. Boston - Uwanja wa Gillette***

Timu inayoutumia: New England Revolution

***Mashabiki: 70,000***

Ulifunguliwa upya mwaka 2002 baada ya kutumika kwenye michuano ya Kombe la Dunia la mwaka 1994.

Uwanja huo uliopo jijini Boston unaweza kuandaa mchezo mmoja wa nusu fainali, ingawa ratiba bado haijathibitishwa.

***3. Dallas - Uwanja wa AT&T***

Timu inayoutumia: Dallas Cowboys (NFL)

***Mashabiki: 92,967***

Uwanja mkubwa zaidi katika NFL, Uwanja wa AT&T wa Dallas umeandaa baadhi ya matukio ya kupendeza na ya hali ya juu katika historia ya michezo nchini Marekani.

Uwanja huu unaweza kuhitaji kupanuliwa ili kuchukua nafasi ya kucheza fainali ya Kombe la Dunia 2026.

***4. Houston - Uwanja wa NRG***

Timu inayoutumia: Houston Texans (NFL)

***Mashabiki: 72,220***

Mechi pekee ya Manchester dabi iliyofanyika nje ya England ilifanyika katika Uwanja wa NRG wa Houston mwaka 2017.

***5. Kansas City - Uwanja wa Arrowhead***

Timu inautumia: Kansas City Chiefs (NFL)

***Mashabiki: 76,640***

Nyumba ya zamani ya Sporting Kansas City, uwanja wa Arrowhead unashikilia rekodi ya uwanja wenye sauti kubwa zaidi kuwahi kutokea.

Kiwango cha sauti cha 142.2 dB kilirekodiwa wakati wa mchezo wa NFL wa mwaka 2014.

***6. Los Angeles - Uwanja wa SoFi***

Timu zinazoutumia: Los Angeles Rams (NFL), Los Angeles Chargers (NFL)

***Mashabiki: 70,000***

Uwanja wa SoFi haukujumuishwa hata katika ombi la awali la Kombe la Dunia, lakini Shirikisho la soka la kimataifa, Fifa, likaomba utumike pia.

Uwanja bado haujaandaa mechi ya mpira wa miguu, kwa mara ya kwanza utatumika kwenye Ligi ya MLS, Agosti mwaka huu.

***7. Miami - Uwanja wa Hard Rock***

Timu zinaozutumia: Miami Dolphins (NFL), University of Miami

***Mashabiki: 67,518***

Marekebisho ya hivi majuzi ya upanuzi wa dola milioni 500 yameufanya Uwanja wa Hard Rock kuwa miongoni mwa viwanja bora zaidi nchini Marekani.

Real Madrid na Barcelona zilitoka suluhu katika mtanange wa Clasico hapa mwaka 2017.

***8. New York/New Jersey - Uwanja wa MetLife***

Timu zinazoutumia: New York Giants (NFL), New York Jets (NFL)

***Mashabiki: 87,157***

Unaweza kuwa na umri wa miaka 12 tu, lakini Uwanja wa MetLife una historia ya kifahari linapokuja suala la kuandaa mechi za mpira wa miguu.

Pande za kimataifa kutoka kote ulimwenguni zimecheza mechi za kirafiki hapa, lakini umeandaa hafla kubwa.

***9. Philadelphia - Lincoln Financial Field***

Timu inayoutumia: Philadelphia Eagles (NFL)

***Mashabiki: 69,328***

Uwanja wa Lincoln Financial Field ni wa aina yake ukiwa umerembwa na paa zinazofunguka.

Pia ulitumika katika mechi ya kirafiki kati ya Manchester United na dhidi ya Barcelona mwaka 2003 ikiwa ni mechi ya kwanza kufanyika hapo.

***10. Francisco - Uwanja wa Levi***

Timu inayoutumia: San Francisco 49ers (NFL)

***Mashabiki 70,909***

Kwa kadiri usasa unavyoendelea, Uwanja wa Levi uko juu na bora zaidi. Una mfumo wake mkubwa wa huduma ya internet (Wi-Fi) na paa kubwa lilliloufunika.

## ISIKUPITE

XAVI Hernandez hajaweza kusafiri na wachezaji wengine wa kikosi cha Barcelona kwenda Marekani na amelazimika kubakia Katalunya kutokana na matatizo ya kiutawala na nyaraka zake. Imeelezwa kuwa Xavi aliwahi kuingia Iran kama mchezaji wa Al Sadd. Marekani imepiga marufuku kwa watu waliokwenda nchini Iran mara nyingi kuingia nchini humo bila kibali maalum.



## Extra Time

# MCHEZAJI BORA WA KILA TAIFA KOMBE LA DUNIA



GARETH BALE

**LONDON,** England

KOMBE la Dunia la 2022 linakaribia kwa kasi huku tukio hilo likitarajiwa kuanza Novemba 21, mwaka huu, nchini Qatar.

**Baada ya kampeni ndefu zaidi ya kufuzu, timu 32 ambazo zitashiriki mashindano hayo zilifahamika Juni.**

Hata hivyo, katika kundi zima la mataifa, kuna nyota wengi wenye vipaji na makala hii inamwangalia mchezaji bora wa kila timu kwenye mashindano hayo.

**Qatar - Akram Afif**

Kidogo kinatarajiwa kwa wenyeji ambao wanajumuisha wachezaji wa nyumbani.

Akram Afif - winga wa zamani wa Villarreal, atahitaji kucheza kwa bidii kuisaidia nchini yake.

**Ecuador - Moises Caicedo**

Mchezaji wa zamani wa West Ham na Valencia, Moises Caicedo ni muhimu zaidi kwa Ecuador.

Kiungo huyo wa kati wa Brighton alikuwa amecheza mechi zaidi ya 20 kabla ya kutimiza umri wa miaka 21.

**Senegal - Sadio Mane**

Sadio Mane atakuwa na matumaini ya kuiongoza timu ya Afrika zaidi ya robo fainali kwa mara ya kwanza katika historia ya Kombe la Dunia.

Ikiwa mtu yeyote anaweza kuibeba Senegal kwenye mabega yake basi ni nyota huyo wa zamani wa Liverpool ambaye kwa sasa yupo Bayern Munich.

**Uholanzi - Virgil van Dijk**

Mabeki wa kati kwa kawaida hawajulikani kama wabadilishaji mchezo, lakini Virgil van Dijk si beki wa kati wa kawaida.

Hakuna hata mmoja katika soka la dunia anayemkaribia Van Dijk katika nafasi yake na atakuwa na hamu ya kuvutia baada ya kukosa michuano mitatu iliyopita.

**England - Harry Kane**

Harry Kane alitwaa Kiatu cha Dhahabu kwenye Kombe la Dunia lililopita na atalenga kufanya hivyo tena huko Qatar.

Kuna alama nyingi za maswali zinazoning'inia kwenye uteuzi wa Gareth Southgate kuelekea dimba, lakini nafasi ya Kane mbele sio mojawapo.

**Iran - Sardar Azmoun**

Misimu kadhaa ya ufungaji bila kufunga nchini Urusi ilipelekea Sardar Azmoun kuhusishwa na uhamisho wa Ligi Kuu ya England.

Alijiunga na Bayer Leverkusen na anasalia kuwa mchezaji muhimu zaidi wa Iran.

**Marekani - Christian Pulisic**

Marekani wamerejea kwenye Kombe la Dunia na matarajio ni makubwa.

Anayekabili shinikizo nyingi atakuwa Christian Pulisic, ambaye hajaonesha ubora wake katika ngazi ya klabu hivi karibuni.

**Wales - Gareth Bale**

Haijulikani ni muda gani ataendelea kucheza baada ya Kombe hili la Dunia, lakini jambo moja ni hakika - Gareth Bale anasalia kuwa hirizi ya Wales.

**Argentina - Lionel Messi**

Kama Bale, Lionel Messi anafikia mwisho wa maisha yake ya soka.

Je, kuna shaka yoyote kwamba yeye bado ni muhimu? Je, anaweza kuibeba Argentina mwaka huu, hilo ni suala la kusubiri kuona.

**Saudi Arabia - Salem Al-Dawsari**

Saudi Arabia inapaswa kuungwa mkono vyema nchini Qatar na mashabiki watakaofanya safari hiyo fupi watafurahi kumtazama nyota wa kimataifa, Salem Al-Dawsari.

Yeye ni mmoja wa kundi teule la wachezaji wa Saudi ambao wamefika Ulaya wakati akitua Villarreal.

**Mexico - Hirving Lozano**

Hirving Lozano huenda ndiye tumaini zuri zaidi la Mexico kuelekea michuano hii.

Mshambuliaji huyu wa Napoli ni mbeba mpira aliyekamilika lakini wakati mwingine hukosa matokeo.

**Poland - Robert Lewandowski**

Wachezaji wachache wa Poland katika mchezo huu wameacha historia, lakini Robert Lewandowski ana nafasi kubwa zaidi ya kutamba.

Kitu kimoja kinachokosekana kwenye taaluma yake ni kuiongoza Poland ndani kabisa ya mashindano. Labda hiyo inaweza kubadilika kipindi hiki.

**Ufaransa - Kylian Mbappe**

Florentino Perez anaweza kumchukia, lakini Ufaransa inampenda.

Baada ya Euro 2020 iliyokatisha tamaa, Mbappe ana uhakika wa kuthibitisha kwenye Kombe la Dunia huku Les Bleus wakiwa wanapewa nafasi kubwa.

**Denmark - Christian Eriksen**

Christian Eriksen ameonyesha dhamira ya ajabu ya kurejea katika ubora wake baada ya kupata mshtuko wa moyo kwenye michuano ya Euro 2020.

Alikuwa mahiri kabisa kwa Brentford katika nusu ya pili ya msimu wa 2021/22.

**Tunisia - Wahbi Khazri**

Hannibal Mejbri anaweza kutwaa taji lake hivi karibuni, lakini kwa sasa, Wahbi Khazri ndiye mshambuliaji bora wa Tunisia.

Fowadi huyo ametumia maisha yake yote nchini Ufaransa.

**Hispania - Pedri**

Wengine wanaweza kusema kuwa ni mapema sana kwa Pedri kuchukuliwa kuwa mchezaji bora wa nchi yake. Tunafikiri vinginevyo.

Kijana huyo anacheza akiwa na ukomavu kama mkongwe mwenye umri wa miaka 30 na huwa anafanya mambo kutokea katika safu ya kiungo.

**Costa Rika - Keylor Navas**

Huenda akicheza Kombe lake la Dunia mara ya mwisho, kipa bora zaidi wa Costa Rica katika historia atakuwa na matumaini ya kuifanya nchi yake kujivunia mnamo Novemba.

Anatazamiwa kuwa na shughuli nyingi na mechi dhidi ya Hispania na Ujerumani katika hatua ya makundi.

**Ujerumani - Joshua Kimmich**

Hakuna mchezaji bora katika kikosi cha Ujerumani - wana nguvu kwa pande zote.

Hata hivyo, Joshua Kimmich ana uwezo wa kuwa tofauti kwenye Kombe la Dunia.

**Japan - Daichi Kamada**

Japan inaweza kuwa farasi mweusi kufika mbali katika Kombe hili la Dunia. Ingawa wanakosa nguvu ya kina, kuna mengi ya kupenda kuhusu 11 yao inayoanza, haswa Daichi Kamada.

Kiungo mshambuliaji anaongoza safu ya wachezaji wa mbele wenye ufundi ambao wataleta matatizo.

**Ubelgiji - Kevin De Bruyne**

Kevin De Bruyne pengine ndiye kiungo bora zaidi duniani na amekuwa kwenye kiwango boda kwa muda mrefu ana nafasi ya kuibeba Ubelgiji.

**Canada - Alphonso Davies**

Kusubiri kwa muda mrefu kwa Canada kushiriki Kombe la Dunia kutakamilika mnamo Novemba shukrani kwa mchango mkubwa wa Alphonso Davies.

Beki huyo wa kushoto wa Bayern Munich atakuwa muhimu katika pande zote mbili kwa upande wake.

**Morocco - Achraf Hakimi**

Hata kama Hakim Ziyech aliichezea nchi yake, mchezaji bora wa Morocco bado ni Achraf Hakimi.

**Croatia - Luka Modric**

Luka Modric asiye na wakati anaonyesha ishara ndogo ya kuachia, lakini hakika hii itakuwa michuano yake ya mwisho.

Modric aliisaidia Croatia katika fainali ya Kombe la Dunia 2018, na kupata tuzo ya Ballon d'Or kwa juhudi zake.

**Brazil - Neymar**

Vinicius Junior anatishia kunyakua nafasi yake, hata hivyo, Neymar anasalia kuwa bora kwa nchi yake kuelekea Kombe la Dunia la 2022.

Atakuwa na hamu ya kuendelea kuwa fiti, jambo ambalo hajawahi kulifanya siku za hivi karibuni.

**Serbia - Filip Kostic**

Huu ni mvutano wa pande tatu kati ya Dusan Tadic, Aleksandar Mitrovic na Filip Kostic.

Hatimaye tumekwenda kwa Kostic, mmiliki wa mguu mtamu zaidi wa kushoto katika soka duniani.

**Uswisi - Yann Sommer**

Sawa na Serbia, Uswizi ina wachezaji kadhaa ambao wanaweza kutwaa taji hili na Yann Sommer ndio nyota wao bora.

**Cameroon - Andre Onana**

Anaweza kuwa na kutu kutokana na kupigwa marufuku kwa dawa za kulevya hivi majuzi, lakini Andre Onana ni mmoja wa makipa bora barani Ulaya.

Atatumaini kuzoea mazingira yake mapya kule Inter kabla ya kutimkia Qatar.

**Ureno - Cristiano Ronaldo**

Ureno imejaa wakongwe, lakini hakuna muhimu zaidi kuliko Cristiano Ronaldo.

Tunadhani rekodi yake inajieleza yenyewe.

**Ghana - Inaki Williams**

Inaki Williams kuitangaza Ghana kabla ya Kombe la Dunia la 2022 ilikuwa ni msaada mkubwa kwa Black Stars.

**Uruguay - Federico Valverde**

Darwin Nunez anakuja kwa nguvu lakini uzoefu wa Federico Valverde katika kiwango cha juu unampa makali.


**Korea Kusini - Son Heung-min**

Wachezaji wachache kwenye orodha hii wako mbele zaidi ya wenzao kuliko Son Heung-min.

Mchezaji huyo wa Tottenham Hotspur ni fowadi halisi wa kiwango cha dunia kama alivyothibitisha mara kwa mara katika misimu ya hivi karibuni.

## Nukuu

"NINA furaha sana kuwa hapa na timu hii Chelsea. "Ni timu kubwa duniani na ndoto yangu ilikuwa ni kucheza Ligi Kuu England, Chelsea walikuja kwanza mwaka 2016 lakini hatukufanikiwa, sasa walipokuja kwangu nilikubali kwa sababu walinihitaji sana." **Kalidou Koulibaly**




"NINGEPENDA kuwashukuru wachezaji wenzangu, wafanyakazi, usimamizi wa kilabu na kila mtu ambaye amekuwa akiniunga mkono kila wakati na kutuwezesha kushinda mataji kwa FC Bayern." **Robert Lewandowski.**



"NINAMUHESHIMU sana Cristiano Ronaldo, mafanikio yake na kazi yake. Lakini kwa mara nyingine tena: Hiyo ilikuwa na sio mada kwetu," alisema Salihamidzic akiiambia Sport." **Mkurugenzi wa Michezo wa Bayern, Munich Hasan Salihamidzic**





# WAGHANA WA5 WALIOTEKA SOKA LA BONGO

Kiungo mshambuliaji mpya wa klabu ya Simba Augustine Okra kutoka nchini Ghana. **PICHA: MTANDAO**

**Na Adam Fungamwango**

USAJILI kwa ajili ya msimu ujao wa mashindano unaendelea kwa klabu mbalimbali nchini, huku klabu za Simba, Yanga na Azam zikishusha wachezaji kutoka Afrika Magharibi.

**Azam pamoja na wachezaji wengine, imekwenda Afrika Magharibi kuwasajili Waivory Coast wawili Kipre Junior, Tape Edinho, Mnaigeria Issa Ndala na Mghana James Akaminko.**

Yanga imesajili wachezaji kadhaa kutoka nje ya nchi, lakini mchezaji iliyomsajili kuelekea msimu ujao kutoka Afrika Magharibi ni Mburkina Faso, Stephane Aziz Ki aliyekuwa akiichezea Asec Mimosas ya Ivyory Coast.

Kwa upande wa Simba, mchezaji pekee kutoka nje ya nchi mpaka sasa ambaye imemsajili ni Augustine Okra kutoka nchini Ghana.

Kuanzia mwanzoni mwa miaka ya 2000, Tanzania imekuwa ikipokea wachezaji wengi kutoka nje ya nchi, lakini leo tutawaangalia waliotoka nchini Ghana.

Pamoja na mambo mengine, wachezaji kutoka nchi hiyo wameonekana kuliteka soka la Tanzania kuliko wa baadhi ya nchi zingine, ingawa mara kadhaa wamekuwa hawadumu kwenye timu moja.

Kwenye makala haya tutawatazama wachezaji kutoka Ghana kama Okra na kukipiga na klabu mbalimbali nchini.

**Kennth Asamoah (Yanga)**

Ni straika hatari aliyekipiga na Yanga 2010 hadi 2012, akitokea nchini Ghana. Ni mmoja wa mastraika waliokuwa tishio si kwenye ligi ya Bongo tu, hadi hata kwenye michuano mingine ya kimataifa.

Ikumbukwe kuwa Asamoah alipa Yanga Kombe la Kagame mwaka 2011 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa alipofunga bao pekee kwenye mechi ya fainali dhidi ya Simba. Ilikuwa ni krosi ya Julius Mrope kwenye wingi ya kushoto, iliyokwenda kutua kwenye kichwa na mfungaji akaujaza wavuni.

Asamoah alifunga bao hilo kwenye dakika 30 za nyongeza baada ya timu hizo kutoka suluhu kwa dakika 90 za mchezo, Yanga ikishinda bao 1-0. Mwaka 2012 akaipa kisogo timu hiyo.

**Yaw Berko (Yanga na Simba)**

Ni mmoja kati ya magolikipa wachache kutoka nje ambao wameacha historia isiyofutika kwenye soka la Tanzania.

Yaw Berko, kipa bora kabisa, mwenye uwezo wa hali ya juu kutoka Ghana, aliichezea Yanga 2009 hadi 2010 kwa mkopo akitokea Liberty Professional ya nchini humo.

Uwezo wake wa kujipanga golini, kuelekeza mabeki jinsi ya kusimama, kuruka, kuokoa michomo na hata kuwakalia mastraika wanapokuwa ana kwa ana na yeye, ilimpa sifa sana.

Hata alipoondoka, Simba ilimfuata na kumrejesha 2014 na uwezo wake ukawa ni ule ule. Alisaini miezi sita na kuongeza sita mingine baadaye na alipomaliza akaondoka.

Mashabiki wa soka wanamfananisha uwezo wa kipa huyo kukaribiana sana na kipa mwingine kutoka nchini Burundi ambaye aliichezea Simba na kuacha jina kubwa, Mackenzie Ramadhani.

**Nicolaus Gyan (Simba)**

Mghana huyu alisajiliwa na Simba kama straika kutoka nchini kwao na alivuma sana na kufanya kazi kubwa kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika mwaka 2017.

Alikuwa mmoja wa wachezaji wenye mchango mkubwa kwa Simba kutinga robo fainali ya Ligi ya Mabingwa kwa mara ya kwanza tangu ilipofanya hivyo mwaka 1994, akicheza beki wa kulia na kuachana na namba yake ya zamani, ushambuliaji.

Alifanya kazi kuanzia mwaka 2017 hadi 2019 alipoachwa na kukaa bila klabu yoyote. Kwa sasa anaichezea Singida Big Stars, akiwa mmoja wa wachezaji waliopandisha daraja msimu huu na msimu ujao ataonekana tena kwenye Ligi Kuu.

**James Kotei (Simba)**

Ni kiungo mkabaji aliyekuwa kipenzi cha mashabiki wa Simba kutokana na aina yake ya uchezaji na kujituma na kuhaha uwanja mzima kuzima mashambulizi ya wapinzani na kulinda mabeki.

Alisajiliwa na Simba 2017 na kuwa mmoja wa wachezaji waliorejeshea heshima timu hiyo kwa kutwaa ubingwa baada ya misimu mitano bila taji. Pia akaipeleka robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Mghana huyu, aliondoka Simba 2019 na kutua klabu ya Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini, lakini kwa sasa yupo Singida Big Stars ambayo msimu unaokuja itacheza Ligi Kuu Tanzania Bara na yeye akiwamo.

**Bernard Morrison (Yanga na Simba)**

Kama ilivyokuwa kwa Berko, Morrison anakuwa Mghana wa pili kuzichezea klabu zote kubwa Tanzania za Simba na Yanga.

Mchezaji huyo mtukutu, lakini mwenye mashabiki wengi kwenye klabu zote mbili, alianza kuichezea Yanga mwaka 2000 kwa miezi sita tu kabla ya kuhamia kwa watani zao wa jadi Simba mwaka huo huo hali iliyozua mtafaruku hadi kupelekana FIFA.

Akiwa Simba, Morrison alibeba timu hiyo kwenye baadhi ya mechi, hasa za kimataifa kiasi cha kuweza kufika hata robo fainali ya Kombe la Shirikisho Barani Afrika.

Mwaka huu amerejea tena kwenye klabu yake ya zamani Yanga, na anatarajia kuonekana akivaa uzi wa njano na kijani msimu wa mashindano utakapoanza.

**JE, WAJUA?**



NAHODHA wa Manchester United, Harry Maguire amekiri kuwa alicheza chini ya kiwango ndani ya kikosi hicho msimu uliopita. Maguire alikuwa na matokeo mabaya msimu wa 2021-22 kiasi cha kocha wa muda Ralf Rangnick kupokea malalamiko ya mashabiki kutaka mchezaji huyo avuliwe unahodha.





# Wakazi wa Ntyuka waitwa kuunganishiwa huduma ya maji

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA), imewataka wakazi wa Ntyuka, kuwasilisha maombi ya kuunganishiwa maji baada ya kukamilika kwa mradi wao wa maji uliojengwa kwa fedha za maendeleo ya ustawi wa taifa na mapambano dhidi ya UVIKO-19.

Mradi wa Ntyuka-Chimala umegharimu Sh. milioni 471.8 kati ya hizo Sh. milioni 359.7 za UVIKO-19 na Sh. milioni 112 zimetolewa na mamlaka hiyo kutoka kwenye vyanzo vyake vya mapato.

Mkuu wa Kitengo cha huduma kwa wateja wa Mamlaka hiyo, Pendo Mkali, aliyasema hayo jana kwenye kikao cha Duwasa na wananchi hao.

Alisema Duwasa kwa kushirikiana na Benki ya Equity inamwezesha mwananchi kuunganishiwa maji kwa mkopo.

"Mradi huu ni mkombozi kwenu tunaomba mtumie fursa hii sasa kuvuta kwenye nyumba zenu," alisema.

Naye Meneja Biashara wa Benki hiyo, Richard Mwambuluma, alisema mwananchi anatakiwa kufika kwenye Ofisi ya Duwasa na kuomba maunganisho mapya na kupewa gharama zote ambazo atapeleka kwenye benki hiyo ili kupata mkopo atakaoulipa ndani ya miezi sita.

"Huu mkopo ni wa masharti nafuu ambao kila mwananchi mwenye kipato cha kawaida anaweza kumudu," alisema.

Awali Mhandisi wa Mradi huo, James Lyoba, alisema mpaka sasa hakuna mwananchi hata mmoja aliyejitokeza kuomba kuunganishiwa licha ya kuwapo na tangi la maji lenye ujazo wa lita 200,000.

Diwani wa Kata ya Ntyuka, Yona Mkobora, aliishukuru Duwasa kwa kukamilisha mradi huo ambao inaonesha namna ilivyojipanga kumsaidia Rais Samia Suluhu Hassan kumtua mama ndoo kichwani.



Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, akipanda juu ya moja ya matangi ya maji kwa ajili ya kuyakagua yaliyojengwa na Kampuni ya Plasco Limited DSM katika kijiji cha Dabalo Wilaya ya Chamwino baada ya kuweka jiwe la msingi wa mradi huo wa maji juzi, (kushoto) ni Naibu Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wawekezaji washauriwa kuwekeza viwanda vya mbolea

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Mbolea nchini (TFRA) imeshauri wawekezaji kuwekeza kwenye viwanda vya mbolea nchini ili kukabiliana na soko la bidhaa hiyo nje na ndani ya nchi.

Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Dk. Stephano Ngailo, alitoa rai hiyo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu soko la bidhaa hiyo ndani na nje ya nchi.

Alisema hivi sasa mahitaji ya mbolea ni makubwa nchini na wawekezaji wa ndani na nje wana fursa ya kuwekeza ili wakulima wapate bidhaa hiyo.

"Naomba wawekezaji mjitokeze kuwekeza katika sekta ya mbolea, naamini mkifanya hivyo mtarejesha kile mlichowekeza ikiwamo na faida kutokana na umuhimu wa bidhaa hiyo," alisema Dk. Ngailo.

Dk. Ngailo alisema kutokana na kuwapo na mahitaji ya mbolea nchini Rais Samia Suluhu Hassan alishafungua mipaka ya uhusiano wa kidiplomasia ya kuvutia uwekezaji wa bidhaa nchini na nyingine.

Alisema kuwa, Tanzania ni kitovu cha mbolea katika Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara (SADC).

"Watu wanaongezeka na ardhi inabaki pale pale lazima tuongeze tija kwa kuzingatia kanuni bora za matumizi sahihi ya mbolea katika kuongeza mapato ya mavuno," alisema.

Naye Kaimu Meneja huduma za sheria kutoka TFRA, Belinda Kesi, alisema wanahamasisha kuzingatia matakwa ya kisheria yaliyowekwa kwenye viwango vya mbolea.

"Kama mdau anataka kuingia katika tasnia ya mbolea ahakikishe anatambulika na mamlaka husika kisheria, jukumu letu ni kusimamia tasnia hii pamoja na majukumu mengine," alisema.

Alifanunua kuwa TFRA imeanzishwa chini ya Sheria namba tisa ya mwaka 2009 ikiwa na jukumu la kusimamia tasnia ya mbolea nchini pamoja na majukumu mengine ni kuhakikisha mbolea hiyo inayotumika, inayoingia, inayosafirishwa nje ya nchi inakuwa katika ubora unaotakiwa na vigezo vya biashara vinazingatiwa.

# Athari kukaa muda mrefu kwenye kiti hii hapa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAFANYAKAZI wanaokaa kwenye viti kwa muda mrefu ofisini, wapo hatarini kuvimba miguu kutokana na kubana mishipa ya damu.

Wameshauriwa kujenga tabia ya kusimama na kufanya mazoezi ya kunyoosha mwili ili kujiepusha kubana mishipa hiyo.

Mtaalamu wa Udhibiti wa Magonjwa wa Wizara ya Afya, Dk. Baraka Nzobo, akizungumza na Nipashe jana, alisema wafanyakazi hususani Makatibu Mahsusi ambao wanakaa zaidi ya saa tatu wanapaswa kutenga muda kidogo wa kutembea ili kuipa nafasi mishipa ya damu kufanya kazi vizuri.

"Kiafya sio vyema mtu kukaa chini zaidi ya saa tatu unapaswa kusimama na kutembea kidogo ili kuipa nafasi mishipa ya damu kufanya kazi yake vizuri ya kusambaza damu na kuepusha tatizo la kuvimba miguu," alisema.

Hata hivyo, Dk. Nzobo alisema, mazoezi ya kufanya sio kukimbia pekee, kutembea ni mazuri hususani kwa mtu ambaye hajawahi kufanya mazoezi.

"Unaweza kuanza na mazoezi ya kutembea umbali mfupi na kadri siku zinavyozidi kwenda unaongeza umbali wa kutembea na mwili ukitoa jasho basi umefanya mazoezi ya kutosha," alisema Dk. Nzobo.

Aliiasa jamii kutambua umuhimu wa kufanya mazoezi kwa muda mchache na baadaye kuendelea na shughuli mbalimbali za ujenzi wa taifa.

"Naomba jamii iwe inafanya mazoezi mara kwa mara ya kusimama, kutembea na kwa wenye uwezo wa kufanya mazoezi ya kukimbia bado yanaruhusiwa na hiyo yote ni kujiweka mwili sawa," alisema Dk. Nzobo.

Mmoja wa wakazi wa Dodoma, Julieth Mosha, alisema amekuwa akifanya mazoezi kila siku ili kuhakikisha afya yake inakuwa vizuri na anafanya ya kutembea pamoja na kukimbia.

Alisema tangu ameanza kufanya mazoezi hayo kwa kufuatilia ushauri wa wataalamu, afya imeimarika ikiwamo kufanikiwa kupunguza uzito uliokuwa hauendani na umri wake.

Alishauri jamii kujiwekea utaratibu wa kufanya mazoezi kila mara ili kujiepusha na magonjwa yasiyo ya kuambukiza.



# CHADEMA yasisitiza kudai Katiba Mpya, Tume Huru

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimeliagiza Baraza la Wanawake wa Chama chicho (BAWACHA), kuendeleza harakati za kudai Tume Huru ya Uchaguzi, ili kuepuka kipengele hicho kuhujumiwa katika mchakato wa Katiba Mpya unaoendelea kwa sasa.

Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, aliyasema hayo juzi jijini hapo wakati wa kongamano la BAWACHA la kudai Katiba Mpya na Tume Huru ya Uchaguzi na kwamba baraza hilo ni nguzo kubwa kwenye mchakato huo.

Alisema kwa sasa nchi nzima watu wanazungumzia Katiba Mpya, lakini kuna wasiwasi kwamba kipengele cha Tume Huru kinaweza kikasahaulika kwa kufunikwa na mambo mengine au kuhujumiwa na watu wasiolitakia mema taifa.

Mnyika alidai baadhi ya viongozi wa serikali pamoja na wanachama wa Chama Cha Mapinduzi wamekuwa wakizungumza kwenye vyombo vya habari wakionyesha kukubaliana na mchakato wa Katiba Mpya, lakini hawana nia njema kama inavyofikiriwa.

Alisema viongozi hao wamekuwa wakisisitiza kuendelea na mchakato wa Katiba Mpya kwa kuanzia na Katiba Pendekezwa ambayo alisema ilishachakachuliwa na kutaka mchakato uanzie kwenye Katiba ya Tume ya Jaji Joseph Warioba.

Alisema Tume Huru ya Uchaguzi ndiyo msingi wa uongozi bora na imara wa taifa na lazima kila Mtanzania mwenye nia njema aipiganie na chama hicho kimekabidhi jukumu hilo kwa BAWACHA.

Alisema Katiba Pendekezwa ambayo viongozi wa CCM wanaitaka bado ina mwendelezo wa Tume ya Uchaguzi kuteuliwa na Rais pamoja na kuapishwa na Rais na endapo mchakato huo utaendelea kuna hatari ya kipengele hicho kuhujumiwa.

"Katiba pendekezwa mbali na kumpa Rais mamlaka ya kuteua na kuapisha Tume ya Uchaguzi, pia imempa mamlaka ya kuteua mpaka Mkurugenzi wa Tume na makamishna, sasa hii haina tofauti kabisa na hii ya mwaka 1977," alisema Mnyika.

Alisema katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 CHADEMA pamoja na vyama vingine vya upinzani vilihujumiwa kutokana na ubovu wa muundo wa Tume ya Uchaguzi.

Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Nyasa, Mchungaji Peter Msigwa, aliwataka wanawake wa chama hicho kuchangamkia fursa ya kugombea ubunge kwenye majimbo ya uchaguzi utakapofika badala ya kutegemea viti maalumu pekee.

Msigwa alisema viti maalumu pekee havisaidii kundi hilo kuwa na uwakilishi mzuri kwenye Bunge kwa kuwa hata kama chama hicho kitashinda majimbo yote nchini bado wanawake wa viti maalumu hawawezi kuzidi 130.

Aliwataka wanawake wa chama hicho kuhakikisha wanajikita katika shughuli mbalimbali zikiwamo za kiuchumi na kijamii ili kukijenga chama katika misingi ya kuwa mbadala wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambacho alisema kimeshindwa kuiendesha serikali," alisema Msigwa.

Alisema serikali imeshindwa kutatua matatizo ya wananchi ikiwamo ukosefu wa ajira kwa vijana, tatizo la maji na mfumuko wa bei za vitu na kuwataka wanawake wa chama hicho kuwasemea wananchi kwenye majukwaa mbalimbali.



Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), John Mnyika, akihutubia Baraza la Wanawake wa chama hicho (BAWACHA) mkoani Mbeya juzi, katika kongamano la kudai Katiba Mpya. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Askari wa kike washauriwa njia za mafanikio

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

ASKARI polisi wa kike mkoani hapo, wameshauriwa kufanya kazi kwa bidii na kwa kuzingatia maadili ya kazi yao ili wapate mafanikio badala ya kuwa na fikra za kuwategemea viongozi kuwabeba au kuwapendelea.

Ushauri huo ulitolewa na aliyekuwa Mkuu wa Jeshi la Polisi wa Wilaya ya Kipolisi Mbalizi, Debora Hokololo, ambaye amepandishwa cheo na kuwa Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani wa Mkoa wa Shinyanga.

Debora alitoa ushauri huo alipokuwa anaagwa na Mtandao wa Maaskari Wanawake Tanzania (TPF Net) Mkoa wa Mbeya pamoja na wadau mbalimbali wa jeshi hilo kuwa hakuna kiongozi yeyote anayeweza kumbeba askari asiyejibiidisha.

Aliwataka wafanye kazi kwa bidii huku wakimtegemea Mungu ili wafanikiwe na kutoa mfano wake kuwa amefanikiwa kwenye majukumu yake kutokana na kuchapa kazi kwa bidii.

"Nawaombeni sana acheni kudeka, acheni kutegemea migongo ya watu, acheni kuita viongozi kwamba ni mibuyu yenu bali fanyeni kazi kwa bidii ili mfanikiwe vinginevyo hamwezi kufanikiwa maana hakuna kiongozi aneyebeba wavivu," alisisitiza Afande Debora.

Alisema, amefanya kazi katika Ukuu wa Polisi Wilaya ya Kipolisi ya Mbalizi kwa muda wa miaka saba na kabla ya hapo alikuwa Mkuu wa Dawati la Jinsia na Watoto katika Ofisi ya Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya.

Majukumu yake mapya ni magumu, lakini alisema atahakikisha anafanya kazi kwa bidii kama alivyofanya kwenye nafasi zingine ambazo amekuwa akizitumikia kabla ili kuhakikisha wananchi wa Mkoa wa Shinyanga wanakuwa salama.

Mtandao huo pia uliwaaga askari mbalimbali wanawake wastaafu utumishi wao na baadhi yao walisisitiza kufanya kazi kwa upendo.

# Serikali kurekebisha mashirika uzalishaji chini ya majeshi

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

SERIKALI imesema inakusudia kuyafanyia marekebisho mashirika ya uzalishaji mali yaliyo chini ya Majeshi ya Polisi na Magereza ili yashirikiane na Taasisi za Kiraia katika kutekeleza miradi mbalimbali ya ujasiriamali kuongeza tija.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa anafunga mafunzo ya awali ya maaskari 700 wa Jeshi la Magereza ambao wamehitimu katika Chuo cha Magereza Kiwira wilayani Rungwe.

Alisema serikali imeshaanza michakato ya kurekebisha mashirika hayo ili kuendana na mfumo mpya wa uendeshaji kwa kushirikiana na taasisi zingine, lengo likiwa ni kuongeza ufanisi katika uzalishaji na uendeshaji. Alisema mageuzi hayo ya mifumo yanahusu uendeshaji pekee wa mashirika hayo na maeneo mengine ya majeshi hayo yatabaki kama yalivyokuwa awali.

"Tumeshaanza kuyafanyia mageuzi mashirika haya ili sasa yaendeshwe kwa mfumo wa ushirikiano kati ya Serikali na Taasisi za kiraia (PPP), lengo la mageuzi haya ni kuongeza tija kwenye uzalishaji na mashirika yanayolengwa ni Shirika la Uzalishaji mali la Magereza na la Polisi," alisema Masauni.

Alisema majeshi hayo yamechagua miradi mitano ya kuiendesha kwa utaratibu mpya utakaoanzishwa ili itumike kama dira kwa miradi mingine itakayoingizwa baadaye.

Masauni aliwataka wahitimu wa mafunzo hayo kujiandaa kwenda kulisaidia taifa kupata maendeleo kwa kwenda kufanya kazi kwa bidii na kwa kuzingatia sheria za majeshi kama walivyofundishwa katika chuo hicho.

Mkuu wa Chuo cha Magereza Kiwira, Kamishna Msaidizi wa Magereza, Rehema Mwailunga, alisema katika mafunzo hayo ya awali askari 700 walihitimu na walikuwa wameandaliwa vizuri kwa ajili ya kwenda kutumika na taifa.

Alisema kati ya wahitimu hao 580 ni wa kike na kwamba wahitimu hao wana ngazi mbalimbali za elimu kuanzia Kidato cha Nne mpaka Elimu ya Chuo Kikuu wakiwa wana ujuzi tofauti.

Alisema askari hao wamefundishwa mbinu mbalimbali za kijeshi na sheria ili wanapokwenda kwenye vituo vyao vya kazi wakafanye kazi kwa weledi na kulisaidia taifa.

"Wahitimu hawa kwa muda ambao tumekaa nao hapa wameonyesha uwezo mkubwa ambao unatupa picha kwamba watalisaidia taifa letu na kwa kuwa wamefundishwa miiko na maadili ya kazi tunaamini watafanya kazi vizuri," alisema Kamanda Mwailunga.

Kamishna wa Magereza Nchini, Suleiman Mzee, alisema askari hao watasambazwa katika maeneo mbalimbali nchini kwa ajili ya kwenda kutumika na kwamba hakuna askari hata mmoja kati yao ambaye atapangiwa kituo katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Aliwataka askari hao ambao asilimia kubwa ni vijana kwenda kufanya kazi kwa bidii na maarifa ili kufikia ndoto zao walizojiwekea.

Nao baadhi ya wahitimu wa mafunzo hayo waliahidi kwenda kufanya kazi kwa bidii na maarifa ili kulisaidia taifa kwa kutumia mbinu walizofundishwa katika chuo hicho.

Mmoja wa wahitimu hao, Mustapha Saddam alisema wamepata maarifa ambayo watahakikisha wanayatumia vizuri kwenye kazi zao pamoja na kuzingatia sheria na maadili ya kazi hiyo.



Baadhi ya watoto wa Kijiji cha Muungoni Kusini Unguja wakicheza katika boti zilizowekwa na wavuvi wa kijiji hicho, eneo la Bahari ya Muungoni. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Rais Mwinyi amsimamisha kazi mkandarasi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amemsimamisha kazi Mkandarasi wa Kampuni ya Associated Investment Company Ltd ya Tanzania inayojenga Shule ya Sekondari ya Mtopepo Zanzibar.

Rais Mwinyi amechukua hatua hiyo baada ya kuona uwezo mdogo wa ujenzi unaoendeshwa na kampuni hiyo ya Dar es Salaam kwa kukiuka masharti ya ujenzi na kuona haja ya kuvunja mkataba.

Katika maelezo yake, Rais Dk. Mwinyi alisema kampuni hiyo tayari imeshachukua muda wa miezi sita, lakini haijafikia hatua za ujenzi kama ilivyokubaliana na serikali na kushangazwa kuomba miezi mengine sita.

Alisema kuwa kampuni hiyo haifai kufanya kazi kwa sababu haina sifa huku akishangazwa na mshauri elekezi, Kampuni ya "Edge Consultacy Company" kushindwa kuishauri serikali jinsi ya utendaji kazi mbovu wa kampuni hiyo na kueleza kwamba kampuni zote hizo hazina sifa wala uwezo. Rais Mwinyi alisema ujenzi wa mradi huo umefikia hatua hiyo kutokana na wizara husika ya elimu na mafunzo ya amali kutokuwa na muhali katika kusimamia miradi ya serikali.

Pia Rais Mwinyi alitoa maelekezo mkandarasi huyo asipewe mradi mwingine wa aina yoyote kutokana na kutokuwa na sifa wala vigezo. "Kampuni haina uwezo, haina bondi na Wizara ya Elimu ndiyo mmetufikisha hapa na hii ndiyo inatokana na yale maneno yanayosemwa kwamba Rais kasema apewe kazi...huyu hafai," alisema.

Alisisitiza haja ya kuchukua hatua kwa kampuni iliyopewa kazi pale inapoonekana utekelezaji wa mradi ya maendeleo haiendi kama ilivyokusudiwa.

Aliwahakikishia wananchi, walimu pamoja na wanafunzi wa shule hiyo mpya ya Sekondari ya Mtopepo kwamba serikali itahakikisha inafanya juhudi ili wakati wa sherehe za Mapinduzi za Januari 12, mwakani shule hiyo inafunguliwa.

Alisema lengo la serikali ni kupunguza idadi ya wanafunzi wengi madarasani na ndiyo maana hatua za makusudi zinachukuliwa kuhakikisha hilo linafanikiwa na kuwataka walimu na wanafunzi kuwa na subira.

Baada ya kuweka jiwe la msingi la Soko la Wajasiriamali linalojengwa kwa fedha za UVIKO-19 huko Shehia ya Munduli, Rais Mwinyi aliitaka Idara ya Manispaa Magharibi 'A' kubadilika na kujikita kibiashara kwa kutafuta fedha na kuongeza vizimba katika soko hilo ili kuleta ustawi wa biashara.

Aliiomba Benki ya CRDB kuendelea kushirikiana na serikali na kuwakopesha fedha wajasiriamali ili kuendeleza biashara zao, huku akiahidi kuongezewa kiwango zaidi cha mitaji vikundi vitakavyofanikiwa kurejesha mikopo ya awali.

Rais Mwinyi alitembelea na kuona maendeleo ya utekelezaji wa mradi wa maji katika eneo la Masingini (Masingini Scheme), unaojengwa na Mkandarasi kutoka Kampuni ya L&T Construction kwa gharama ya Dola milioni 35.8, unaohusisha ujenzi wa matangi mawili ya maji yenye uwezo wa ujazo wa lita milioni 18.

Akizungumza na wananchi wa maeneo ya mradi, Dk. Mwinyi alimpongeza mkandarasi huyo kwa kuendelea na mradi huo vizuri na kuwataka watendaji wa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) kuhakikisha miundombinu hiyo inaleta matumaini mema kwa wananchi katika upatikanaji wa huduma hiyo.

Katika hatua nyingine, Rais Dk. Mwinyi alipongeza mafanikio yaliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika wilaya hiyo ya Magharibi 'A' kupitia sekta za maji, afya, elimu, barabara pamoja na soko la wajasiriamali na kusema anaridhishwa na utekelezaji wa miradi hiyo, mbali na kasoro iliojitokeza kwa mkandarasi anaejenga mradi wa Shule ya Sekondari Mtopepo.

# Jamii yatakiwa kuenzi thamani ya watoto yatima

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Taasisi ya NURU Foundation, Zainab Kombo Shaib, amesema jamii inajukumu kubwa la kuijua na kuienzi thamani ya watoto yatima.

Zainab ambaye ni mke wa Makamu wa Kwanza wa Rais, aliyasema hayo mjini hapo, wakati akizungumza katika kikao cha tathmini ya hafla ya dua ya kuiombea nchi na dhifa ya chakula cha mchana kwa ajili ya watoto yatima iliyofanyika mwishoni mwa wiki iliyopita.

Alisema dhamira kuu ya taasisi hiyo ni kuwasaidia watoto yatima na jamii kwa ujumla na sio kujinufaisha kiuchumi.

"Wapo watu wasio waaminifu wanatumia mwamvuli wa mtoto yatima kama njia ya kujinufaisha kiuchumi, lakini katika taasisi yetu ya Nuru hilo halipo na sitokubali liwepo kabisa," alisisitiza Mwenyekiti huyo wa Nuru Foundation.

Aliwataka wafadhili mbalimbali na jamii kwa ujumla, kuendelea kuisaidia taasisi hiyo ambayo ina idadi kubwa ya watoto yatima na wenye mazingira magumu ambao wanahitaji huduma za kila siku.

Alisema kuwasaidia watoto hao kutawafanya kuishi bila ya majozi na huzuni kutokana na kuondokewa na wazazi wao na kuwa sehemu ya watoto wengine ambao sio yatima. Wadau mbalimbali wa kikao hicho wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Taasisi ya MUZDALIFA Farouk Hamad Khamis, walitoa maoni yaliyoonesha dhamira ya kuunga mkono na kuendeleza juhudi za taasisi hio.

Alisema wapo tayari kuisadia taasisi hiyo ambayo ina mchango mkubwa katika kusaidia makuzi na malezi ya watoto yatima ili kupata huduma zote zinazostahiki ikiwamo elimu.

# UNDP, ACT-Wazalendo wakutana kutathmini siasa 2025

**Na Mwandishi Wetu**

TUME ya Umoja wa Kitaifa ya Shirika la Maendeleo la UNDP, imekutana na viongozi wa Chama cha ACT-Wazalendo kwa lengo la kutathmini hali ya kisiasa na jinsi ya mwenendo wa uchaguzi wa 2025 nchini.

Mwenyekiti wa Chama cha ACT-Wazalendo, Juma Duni Haji, alisema hayo badaa ya kikao kilichofanyika katika ofisi kuu ya chama, Vuga mjini Zanzibar.

Duni alisema ujumbe huo umekuja kuangalia ni maeneo gani yanaweza kusaidiwa katika chaguzi zijazo za mwaka 2025 ziwe huru na zenye kukubalika chini ya usimamizi wa Tume Huru ya uchaguzi.

"Umoja wa Mataifa unaweza kutusaidia ili uchaguzi ujao uwe wa amani, uwe huru na wenye kuaminika katika mwenendo wa kuendeleza siasa za kidemokrasia nchini," alisema Duni.

Aidha, alisema Chama cha ACT-Wazalendo kinahitaji kutekeleza maridhiano ya kweli yaliyokubaliwa na aliyekuwa Mwenyekiti wa chama hicho, marehemu Seif Sharif Hamad pamoja na Rais wa Zanzibar, Dk. Husein Mwinyi.

Ujumbe wa UNDP ukiongozwa na mwakilishi kutoka Umoja wa Mataifa, Akinyeni Adegbola, alisema watafikisha ripoti katika ofisi yao na kueleza ni maeneo gani watasaidia ili chaguzi ziwe za amani huru na haki.

# Zijue sheria, kanuni na haki za kupata habari

**Na Mwandishi Wetu**

## • MCT yatoa mwongozo wa kufuatwa • Yako madhila yanayowakumba waandishi wa habari na vigingi



Rais wa Baraza la Habari Tanzania (MCT), Jaji Juxon Mlay (wa pili kulia), Katibu Mtendaji wa MCT, Kajubi Mukajanga (wa pili kushoto), Mjumbe wa Bodi ya MCT, Tido Mhando (kushoto) na Mkufunzi wa Vyombo vya Habari, Rose Mwalimu, wakionyesha ripoti kuhusu mwongozo wa vyombo vya habari wa kuandika habari za watoto, wakati wa hafla ya uzinduzi wa machapisho manne ya baraza hilo, uliyofanyika jijini Dar es Salaam. **PICHA: MIRAJI MSALA**

BARAZA la Habari Tanzania (MCT) limezindua machapisho manne ya vitabu vinavyotoa miongozo kwa waandishi wa habari, maofisa habari na wananchi kupata na kutoa taarifa kwa usahihi.

Katika kitabu cha Mwongozo wa Kupata Taarifa kwa Waandishi wa Habari na Maofisa Habari, Baraza hilo limebainisha sheria, kanuni, haki ya kupata taarifa na kutoa taarifa kwa waandishi wa habari, maofisa habari na wananchi kwa ujumla ili kujua wajibu wao katika kupata na kutoa habari.

Kutokana na umuhimu wa upatikanaji wa taarifa ambao umetajwa katika mwongozo wa namna ya kupata habari ili kukidhi haja na matakwa ya kuwawezesha maofisa habari kutoa taarifa kwa mujibu wa sheria, waandishi wa habari hawana budi kufuata sheria katika kutafuta taarifa wezeshi kwa vyombo vya habari ili kutimiza wajibu wao kama Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inavyoelezea kupitia Sheria ya Haki ya Kupata Taarifa.

Baraza la Habari linaamini kwamba ni muhimu kuwa na miongozo na sheria zitakazoleta haki na usawa katika upatikanaji taarifa na utoaji, hasa kwa waandishi wa habari, maofisa habari na wananchi kwa ujumla.

### SHERIA NA KANUNI

Septemba 7, 2016, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilipitisha Sheria ya Upatikanaji wa Taarifa inayowapatia wananchi haki ya kupata taarifa kutoka serikalini na katika sekta binafsi.

Sheria hii inatumika Tanzania Bara pekee.

Sheria hii iliyotungwa na Bunge inayotoa maelekezo ya namna na haki ya kupata taarifa, inapanua wigo na uwazi kwa jamii namna ya kupata na kutoa taarifa katika taasisi za umma na zile za binafsi ili jamii iweze kuzipata kwa uwazi na kwa uhakika.

Aidha, uwapo wa sheria hii katika nchi umekuwa na matokeo chanya, ikiwawezesha wanahabari kuibua kero nyingi katika sekta mbalimbali kama ubadhirifu serikalini na sekta binafsi, rushwa, uovu katika jamii; ukatili wa kijinsia unaoshuhudiwa sasa kila wakati ukiripotiwa na vyombo vya habari na kusaidia wananchi, ambao sasa wamekuwa wepesi kutoa taarifa yoyote inayowasibu.

Mfano; hapa nchini sasa serikali imekuwa na kipindi maalum cha kuzungumza na wananchi kila mwezi kupitia Televisheni ya Taifa (TBC), Msemaji wa Serikali anapokea simu za wananchi mbalimbali ili kujibu kero na changamoto zinazowakabili kutoka sehemu tofauti.

Hii ni kudhihirisha umuhimu wa sheria hii na wananchi wanaweza kunufaika nayo kwa sababu upatikanaji wa taarifa una tija kubwa kwa serikali na wananchi.

Sheria ya Haki ya Kupata Taarifa ni fupi na ina vifungu vichache vya awali, ambavyo vinatoa tafsiri ya maneno yanayotumika ikilinganishwa na sheria nyingine za nchi. Sheria hii imegawanyika katika sehemu nne na vifungu 24.

Sehemu ya kwanza ina vifungu vya awali, ambavyo vinatoa tafsiri ya maneno yanayotumika katika sheria hiyo, sehemu ya pili inazungumzia haki ya kupata taarifa, sehemu ya tatu; upatikanaji wa taarifa na sehemu ya nne; vifungu vinavyotoa masharti ya jumla.

Aidha, sheria hii inatoa mwongozo wa kupata taarifa na haki ya kutoa taarifa kwa uwazi katika nyanja zote za mtoaji taarifa na mpokeaji bila kuvunja sheria na kanuni zake. Kutokana na mwongozo huu, sheria imeweka mwenendo madhubuti wa uombaji na ushughulikiaji wa maombi ya taarifa ambao ni rahisi, bure na wa haraka.

Mwenendo huu unaelezewa katika vifungu vya 10, 11, 12, 13, 14, 15, 16, 17, 18 na 19 vya sheria hii. Vifungu hivi vinaeleza pamoja na mambo mengine pia namna maombi ya kupata taarifa yanavyopaswa kuandaliwa, utoaji wa notisi ya upatikanaji wa taarifa usizidi ndani ya siku 30, namna ya upatikanaji wa nyaraka nyingine ambazo hazikuombwa na mtoaji taarifa, pia namna ya kuhamisha maombi ya upatikanaji wa taarifa.

Aidha, vifungu hivyo vinaelezea kinachopaswa kufanyika iwapo mtoa taarifa hatatimiza wajibu wake, namna ambavyo taarifa inaweza kutolewa na pia namna ambavyo taarifa iliyoombwa inapaswa kutumika.

Sheria imetoa mazingira machache yanayoruhusu uminywaji wa taarifa ili kuzuia madhara, kulinda usalama na maslahi ya umma.

Hii inatamkwa chini ya kifungu cha 6 cha sheria. Kifungu cha 6(2) na (3) kinatoa mazingira ambayo taarifa zinaweza kuminywa au kuzuiwa. Kwa mfano taarifa zinazohusu uhusiano wa Tanzania na nchi za nje au shughuli za nje (foreign activities) kutambuliwa kama ni taarifa za usalama.

Sheria hii imempa haki ya kukata rufani mwomba taarifa endapo hajaridhika na huduma kuhusu maombi yake ya taarifa. Hii inatamkwa chini ya kifungu cha 19(4) cha sheria. Kifungu hiki kinampa mtu haki ya kukata rufani katika Mahakama Kuu, iwapo mtoa taarifa atakataa kutoa taarifa kwa mwombaji wa taarifa.

Ulinzi dhidi ya uvujishaji au utoaji wa taarifa kwa nia nzuri na adhabu dhidi ya kuzuia upatikanaji wa taarifa. Hii inaelezewa chini ya kifungu cha 23(1) na (2) cha sheria hii.

Adhabu dhidi ya ofisa anayezuia upatikanaji wa taarifa inatolewa chini ya kifungu cha 22, ingawaje adhabu hizi ni kwa ajili ya mtu mwingine atakayezuia utoaji wa taarifa na siyo mwenye taarifa mwenyewe.

Vifungu vya 23 na 24 vya Sheria ya Haki ya Kupata Taarifa vinalinda watoa taarifa za maovu kwa nia njema ili kuzuia mtoa taarifa asidhurike kwa namna yoyote. Pia upatikanaji wa taarifa umeminywa kwa watu wasio raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya kifungu cha 5(4). Mbaya zaidi, kuna mazingira mapana ya uzuiaji wa taarifa chini ya kifungu cha 6(2).

Machi, 2021, Baraza la Habari Tanzania lilifanya utafiti katika mikoa sita; Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza, Kilimanjaro na Mtwara ili kujua hali ya upatikanaji wa taarifa wakati wa kipindi cha Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 na katika mazingira ya mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19. Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa wengi wa wanahabari waliohojiwa walionekana kutoijua Sheria ya Haki ya Kupata Taarifa ya Mwaka 2016 na hata Kanuni zake za Mwaka 2017, na kusababisha waandishi wa habari wengi kukutana na madhila mbalimbali wakati wa kuripoti na kupata taarifa, ikiwamo kunyimwa taarifa kutoka taasisi za umma na baadhi ya taasisi binafsi.

### VIKWAZO KWA WAANDISHI

Utendaji kazi wa waandishi wa habari duniani kote unahusisha kutafuta, kukusanya, kuchakata, kuhariri na kusambaza habari ambazo wakati zinatafutwa zilikuwa katika hatua ya taarifa.

Katika kutekeleza majukumu hayo kuna changamoto nyingi ambazo waandishi wa habari wanakutana nazo wakati wa kupata taarifa kutoka vyanzo mbalimbali vya habari. Kutokana na changamoto zote lakini ukweli ni kwamba waandishi wa habari na maofisa habari wengi wao hawajui sheria na kanuni zake za kupata taarifa (Access to Information Act-2016), ambayo imeelezea nini kinatakiwa kufanyika kwa pande zote mbili yaani mtoa taarifa na mpokea taarifa.

Ukweli huu unathibitika kutokana na idadi kubwa ya waandishi wa habari kuendelea kutumia utaratibu wa zamani wa utafutaji wa taarifa uliokuwa ukitumika kabla ya kuwapo kwa Sheria ya Haki ya Kupata Taarifa, yaani waandishi wa habari kuandika maswali kwenye karatasi za ofisi na kuyatuma kwenye ofisi husika au kwa kupiga simu bila kwenda kwenye eneo la tukio (field).

Au wengine kuchukua taarifa kwenye mitandao bila kuzithibitisha sehemu husika, ambapo wao huzitoa taarifa hizo kwenye vyombo vyao na kusababisha mtafaruku na serikali au kwa wananchi.

Aidha, tangu kusainiwa kwa sheria hii ambayo ilipitishwa na Bunge Septemba 7, mwaka 2016 na kuidhinishwa na aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, John Pombe Magufuli, Septemba 23, 2016, njia hizo wanazotumia waandishi wa habari hazifuati matakwa ya sheria.

Hivyo, umakini na uweledi wa waandishi wa habari na maofisa habari utasaidia kuongeza na kuimarika kwa ufanisi katika upatikanaji wa taarifa.

Kikwazo kingine ni waandishi wa habari kunyimwa taarifa, wamekuwa wakinyimwa taarifa za msingi hasa serikalini, lakini tatizo liliko hawatoi taarifa katika Baraza la kunyimwa taarifa hizo. Usiri huo unafanya kazi kuwa nguvu kutokana na kuvunjwa kwa sheria kwa makusudi.

Pia vitisho, mwandishi anapoandika habari ambazo hazifurahishi kwa baadhi ya viongozi mara nyingi hupata vitisho aidha kwa kupelekwa polisi au kuzuiwa kwa namna yoyote, kwa kuwekwa mahabusu au kufukuzwa kazi.

Unyanyasaji, kukamatwa, vipindi kuondolewa hewani, yote hayo ni madhila anayopata mwandishi wakati wa kupata taarifa na kutoa taarifa kwa jamii.

Hivyo, kuna ulazima kwa waandishi wa habari kujua Sheria ya Haki ya Kupata Taarifa na Kanuni zake ili kufanya kazi kwa weledi.

### MWONGOZO UNASEMAJE?

Mwandishi wa habari au mwananchi atatakiwa kujaza fomu inayopatikana kwenye kanuni za Sheria ya Haki ya Kupata Taarifa za mwaka 2017, fomu hiyo itajazwa kutokana na maombi ya taarifa unayoitaka kwenye taasisi husika na mpokeaji wa taarifa atajibu fomu hiyo ya maombi kutokana na takwa la taarifa kwa kuzingatia kanuni za taarifa, na kama taarifa hazitapaswa kutolewa kwa kuzingatia usalama labda wa taifa basi utapaswa kupewa sehemu tuu ya taarifa zitakazostahili kutoka.

Hivyo, ofisa habari atatakiwa kukutaarifu kuwa; sehemu ya taarifa tu ndio utakayopewa, sababu ya kukupa sehemu ya taarifa uliyoomba, jina na cheo cha mtu aliyetoa maamuzi hayo, haki yako ya kufanyiwa mapitio ya sehemu ya taarifa uliyoomba na mtoa taarifa atatakiwa kutoa taarifa katika muda usiopungua siku 30 tangu alipopokea maombi ya taarifa.

### WAJIBU WA OFISA HABARI

Ni muhimu kwa ofisa habari kufahamu kwamba, utoaji na upatikanaji wa taarifa ulikuwapo kwa mujibu wa sheria hata kabla ya kuwapo kwa Sheria ya Haki ya Kupata Taarifa ya Mwaka 2016.

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kifungu cha 18 kinasema: a) ana uhuru wa kuwa na maoni na kujieleza maoni au mawazo yake; b) ana haki ya kutafuta, kupokea na kusambaza taarifa bila ya kujali mipaka ya nchi; (c) ana uhuru wa kuwasiliana na haki ya kulindwa dhidi ya kuingiliwa kati kwa mawasiliano yake; na (d) ana haki ya kupata taarifa wakati wote kuhusu matukio mbalimbali muhimu yanayoendelea kuhusu maisha na shughuli mbalimbali.

Hivyo, ofisa habari anapaswa kuzingatia sheria ya upatikanaji wa taarifa kwa kuzingatia kifungu cha 5(1) kinasema, kila mtu ana haki ya kupata taarifa iliyopo ndani ya mamlaka ya mtoa taarifa, 5(2) kila mtoa taarifa ana wajibu wa kutoa taarifa iliyopo ndani ya mamlaka yake kwa umma hata kama taarifa yake haijaombwa".

Kanuni zinaratibu utekelezaji wa Sheria ya Haki ya Kupata Taarifa, si budi kila ofisa habari anapaswa kutoa taarifa zinazohitajika kwa mwomba taarifa kwa kufuata misingi na sheria husika.

### KANUNI ZA MAADILI

Kwa mujibu wa Sheria ya Haki ya Kupata Taarifa ya Mwaka 2016, kila mtu ana haki ya kupata taarifa, lakini wakati huohuo, kwa tasnia ya habari kuna kanuni za maadili ya waandishi wa habari zinazoiongoza tasnia katika utendaji kazi.

Waandishi wa habari wanapaswa kuzingatia kanuni na maadili ya tasnia kama ukweli wa taarifa, kutoingiza maslahi binafsi kwenye taarifa, kujua wajibu na uwajibikaji katika tasnia, uaminifu na uweledi wa vyombo vya habari, usahihi na uhakiki, haki na usawa, haki ya kujibu, masahihisho, uzingatiaji jinsia na mengineo.

Aidha, katika uzinduzi wa machapisho ya MCT, Rais wa Baraza la Habari Tanzania, Jaji Juxon Mlay, aliwakumbusha waandishi wa habari na jamii kuvisoma vitabu badala ya kuvichukua na kuvifungia kwenye makabati huku wakiacha madini yaliyomo kwenye vitabu hivyo yakipotea bure.

HABARI KIMATAIFA

## Kadhaa wauawa shambulio Togo

**SAVANES,** Togo

MAOFISA nchini Togo wamesema kuwa watu kadhaa wameuawa na wengine kujeruhiwa wakati washambuliaji walipovamia vijiji vinne siku chache zilizopita ambapo uasi wa makundi ya itikadi kali unaenea kutoka mpaka wa Burkina Faso.

Kwa mujibu wa taarifa ya jeshi la nchi hiyo iliyotolewa jana shambulizi hilo lilisababisha vifo na majeruhi kadhaa ambao walishughulikiwa kwa haraka na kundi la kwanza la jeshi hilo lililofika katika eneo la uvamizi.

Aidha, vyombo vya habari nchini Togo, vimeripoti kufariki kwa watu 10 hadi 15. Shambulizi hilo ni la nne kutokea nchini humo tangu mwaka 2021 wakati taifa hilo, Benin, Ghana na Ivory Coast zikikabiliwa na tishio linaloongezeka kutoka kwa wanamgambo wa itikadi kali katika eneo la Sahel kaskazini mwa mipaka yao.

Pia Benin, Togo, Ghana na Ivory Coast zina mipaka ya pamoja na Mali, Niger na Burkina Faso, ambapo operesheni za makundi ya itikadi kali zimesababisha vifo vya maelfu ya watu huku wakazi zaidi ya milioni mbili wakitoroka makazi yao. **DW**

## Moto wateketeza msitu Ulaya

**UFARANSA,** Ulaya

WIMBI la joto kali la msimu wa kiangazi ambalo limesababisha matukio makubwa ya moto kote kusini magharibi mwa Ulaya linaendelea kusambaa, huku maeneo kadhaa ya bara hilo yakijiandaa kwa viwango vya juu vya joto.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa na DW jana, zima moto nchini Ufaransa, Ureno, Hispania na Ugiriki wanapambana na matukio ya moto ya msituni ambao unateketeza maelfu ya hekta ya ardhi na kuwaua maofisa kadhaa tangu mwanzoni mwa wiki iliyopita.

Taarifa inasema hilo ni wimbi la pili la joto kuyakumba maeneo ya kusini magharibi mwa Ulaya katika wiki kadhaa huku wanasayansi wakilaumu mabadiliko ya tabia nchi na kutabiri matukio ya mara kwa mara na makali ya hali mbaya ya hewa.

Aidha, zimamoto katika mji wa pwani wa Arcachon katika jimbo la kusini magharibi la Ufaransa la Gironde wanapambana kuyadhibiti matukio mawili ya moto ya msituni ambao umeteketeza hekta 10,000 tangu Jumanne.

Luteni Kanali Olivier Chavatte kutoka idara ya moto na uokozi, alisema kazi ya kuzima moto huo ni ngumu na wamepeleka zima moto 1,200 na ndege tano ili kuukabili.

Alisema tangu Jumanne ya wiki iliyopita, zaidi ya watu 1400 wakazi na watalii kwa pamoja walilazimika kuondoka huku vituo vya muda vikitengenezwa kuwapokea wanaohamishwa. **DW**

# Marekani yaahidi ushirikiano na Mashariki ya Kati

**JEDDAH,** Saudi Arabia

RAIS wa Marekani, Joe Biden, amemaliza ziara ya siku nne Mashariki ya Kati ambako amewahakikishia viongozi wa nchi za Kiarabu kwamba Marekani itaendelea kushirikiana kwa dhati na mataifa hayo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa na VOA, Biden aliyasema hayo katika mkutano uliofanyika juzi mjini Jeddah, Saudi Arabia ulioongozwa na mwana mfalme Mohammed bin Salman, pamoja na viongozi wa nchi sita wa Baraza la Ushirikiano wa Nchi za Ghuba, (GCC), Misri, Jordan na Iraq.

Rais Biden alisema Marekani haitaondoka kutoka kanda hiyo na kuacha nafasi kuchukuliwa na mataifa mengine kama China, Urusi au Iran.

**Pia Rais Biden pamoja na mwana mfalme Mohammed walishuhudia kutiwa saini mikataba 18 kati ya nchi zao mbili kuhusiana na ushirikiano wa nishati, anga za juu, afya na uwekezaji.**

Biden akiwa katika ziara yake ya kwanza ya Mashariki ya Kati tangu kuchukua madaraka mwezi Januari mwaka 2021, amekuwa akijaribu kuzungumzia namna ya kuzuia kupanda kwa bei za mafuta na kueleza mawazo ya mikakati ya Washington katika kanda zima.

Aidha, taarifa baada ya mkutano huo haikueleza bayana matokeo yaliyopatikana, lakini inadaiwa Biden hakufaulu kupata uhakikisho kutoka kwa viongozi wenzake wa nchi za kiarabu juu ya kuongeza uzalishaji mafuta wala kuitisha mkutano wa viongozi juu ya kuunda muungano utakaoihusisha Israel, wa kupambana na vitisho vya Iran.

Wakati wa mkutano wa ana kwa ana na mwana mfalme Mohammed, Biden alisema walizungumzia masuala nyeti kuhusu haki za binadamu, kuondoa ukosoaji dhidi ya mwana mfalme na ushirikiano kati ya nchi zao mbili.

Pia Rais Biden pamoja na mwana mfalme Mohammed walishuhudia kutiwa saini mikataba 18 kati ya nchi zao mbili kuhusiana na ushirikiano wa nishati, anga za juu, afya na uwekezaji.

Biden pia ameahidi dola bilioni moja ya msaada wa chakula kwa nchi za Mashariki ya Kati. **VOA**



Rais wa Marekani, Joe Biden, akiwa katika kikao cha pamoja na viongozi wa nchi za Kiarabu wakijadili usalama na maendeleo. **PICHA: VOA**

## Saudia, yahadharisha sera zinazoleta mfumuko wa bei

**JEDDAH,** Saudi Arabia

MRITHI wa kiti cha ufalme wa Saudi Arabia Mohammed bin Salman ameonya kuwa sera zisizo za kweli za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi zitasababisha viwango visivyo vya kawaida vya mfumuko wa bei.

Akizungumza katika mkutano wa kilele kati ya Marekani na nchi za Kiarabu uliofanyika jana mjini Jeddah, mwanamfalme huyo alitoa wito wa uwekezaji zaidi katika teknolojia ya mafuta na nishati safi.

Alisema Saudi Arabia itaongeza uwezo wake wa uzalishaji wa mafuta kufikia mapipa milioni 13 kwa siku ifikapo mwaka 2027 kutoka karibu milioni 12 yanayopatikana kwa sasa, huku ikidaiwa kuwa baada ya hapo taifa hilo la kifalme halitaweza kuongeza uzalishaji zaidi. **DW**

## Gazprom yailaumu Siemens mtambo wa usambazaji gesi

**MOSCOW,** RUSSIA

KAMPUNI kubwa ya nishati ya Russia Gazprom imeilaumu kampuni ya uhandisi ya Ujerumani Siemens kwa kukosekana kwa sehemu muhimu ya mtambo unaohitajika kuanzisha tena usambazaji wa gesi asilia barani Ulaya.

Mashine hiyo inayotumika katika bomba la gesi la Nord Stream 1 linalotokea Russia hadi Ulaya, kwa sasa iko nchini Canada kwa ukarabati, huku Gazprom ikiitaka kampuni hiyo ya Siemens kutafuta ruhusa ya kuondolewa kwa mashine hiyo Amerika ya Kaskazini.

Pia Canada inasisitiza kuwa mashine hiyo haikuorodheshwa katika vikwazo vya Magharibi dhidi ya Russia kutokana na vita nchini Ukraine.

Mvutano huo unatokea wakati mradi wa bomba la Nord Stream 1 unaoendelezwa katika bahari ya Baltic ukiwa umesimamishwa kwa siku 10 kwa huduma ya kila mwaka ya kuuboresha.

Aidha, Ujerumani ina wasiwasi kwamba Russia inaweza kutumia kusimamishwa kwa mradi huo kwa muda ili kupunguza kabisa usambazaji wa gesi kwa Ulaya.

**DW**

# MKAZI WA MANYARA ANOGESHA MKATABA WA SIMBA NA M-BET

Na Mwandishi Wetu

MKAZI wa Mkoa wa Manyara, Maraba Masheku, ameshinda Sh. 106, 809, 410 baada ya kutabiri kwa usahihi mechi 12 za ligi mbalimbali za soka duniani kupitia droo ya M-Bet Tanzania ya Perfect 12.

**Masheku ambaye ni shabiki wa Simba na Chelsea alisema haikuwa kazi rahisi kwake kushinda kiasi hicho cha fedha kutokana na ugumu wa kutabiri baadhi ya timu zilizokuwa zikicheza.**

Alisema mechi iliyompa wakati mgumu ni kati ya Uholanzi na Sweden katika mashindano ya Euro ya Wanawake, lakini alifanikiwa kutabiri matokeo sahihi. Kwa mujibu wa Masheku, timu hizo mbili zote ni nzuri na ilikuwa vigumu kutabiri kwani uwezo wao unalingana.

"Nilikuwa njia panda kutabiri matokeo, hata hivyo, nilitumia uzoefu wangu katika kubashiri mechi na kutabiri matokeo kwa usahihi," alisema. "Nimefurahi kuwa mshindi wa kwanza wa droo ya Perfect 12 baada ya M-Bet Tanzania kusaini mkataba wa miaka mitano na timu yangu ya Simba. Ni historia kwangu na kumbukumbu ambayo sitaisahau," aliongeza.

Alisema fedha hizo atazitumia kuboresha biashara yake kwa kuongeza mtaji na vilevile kupanua mtandao wake katika soko.

"Mimi ni mjasiriamali, nina ujuzi wa kuanzisha biashara. Kwa hivyo najua jinsi ya kutumia fedha katika kuanzisha uwekezaji mdogo. Ninapaswa kuwa makini sana na jambo hilo kwa sababu unahitaji kuchambua aina ya biashara, manufaa yake na changamoto kabla ya kuamua chochote."

Mkurugenzi wa Masoko wa M-Bet Tanzania, Allen Mushi, alisema Masheku anaungana na washindi wengine wa droo ya Perfect 12 waliofanikiwa kubadili maisha yao baada ya kujishindia mamilioni ya fedha. Mushi pia amewataka Watanzania wenye umri kuanzia miaka 18 kuendelea kuweka dau lao kwa M-Bet ili kujishindia mamilioni ya fedha.




Mkazi wa Manyara, Maraba Masheku akipozi baada ya kukabidhiwa mfano wa hundi ya Sh. 106,809,410 kutoka kampuni ya M-BET Tanzania baada ya kutabiri kwa ufasaha matokeo ya mechi 12 za mashindano mbalimbali duniani kupitia mchezo wa kubashiri wa Perfect 12. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Pluijm, Singida Big Stars mambo safi

Na Saada Akida

UONGOZI wa Singida Big Stars umemalizana na makocha wawili, Hans Pluijm kuwa kocha mkuu akisaidiana na Mathias Lule kwa mkataba wa miaka miwili kukinoa kikosi cha timu hiyo kwa msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Tayari makocha hao wameanza kazi kukinoa kikosi cha timu hiyo ambayo imeanza mazoezi rasmi katika uwanja wa chuo cha Polisi, Temeke Barabara ya Kilwa, Dar es Salaam.

Pluijm aliyewahi kufundisha Yanga na Singida United misimu tofauti na Lule alikuwa Kocha Mkuu wa Mbeya City msimu huu ulioisha wa ligi hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Lule aliweka wazi kumalizana na tayari amesaini mkataba wa kuwa kocha msaidizi wa Singida, akimsaidiana na Pluijm kwa ajili ya kukinoa timu hiyo.

"Ni kweli nimesaini mkataba na Singida Big Stars, baada ya mkataba wangu na Mbeya City kufikia mwisho lakini ofa yao ilikuwa ndogo zaidi ya sasa niliyopata hapa," alisema kocha huyo.

Licha ya Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Singida Big Stars, Hussein Massanza, kutoweka wazi kuhusu makocha hao, lakini chanzo chetu cha habari kutoka ndani ya bodi hiyo kilisema kwamba kigogo mmoja ndani ya bodi hiyo alikutana na makocha hao kwa ajili ya kumalizana nao kwa ajili ya utaratibu za kusaini mkataba.

Alisema makocha hao wameshaanza kazi ya tangu juzi baada ya kukabiliana na jana wamekamilisha taratibu zote za kusaini mkataba wa kuinoa timu hiyo.

"Tayari Pluijm na Lule sasa ni makocha wa halali wa Singida Big Stars, wameanza kazi rasmi juzi na kufanya mazoezi katika Uwanja wa Chuo cha Polisi kabla ya kikosi kwenda Arusha kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya wa Ligi Kuu," alisema kigogo huyo.



# Mtupa: Ligi Kuu itakuwa ngumu

Na Cheji Bakari, TANGA

KOCHA Msaidizi wa Prisons, Shabani Mtupa, ametabiri Ligi Kuu Bara msimu ujao 2022/23 itakuwa na ushindani mkubwa zaidi ya uliopita.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu amebainisha sababu mbalimbali ikiwamo maandalizi ya timu na zawadi zinazotolewa kwa mshindi wa kwanza hadi wa kumi na mbili kuwa ndio chachu ya ligi kuwa ngumu.

"Kama sisi Prisons msimu huu hatukutarajia kufanya vibaya, lakini kutokana na ushindani tulioupata tumejifunza kitu, hii inaonesha kuwa msimu wa 2022/23 utakuwa mgumu zaidi," alisema.

"Ukiangalia msimu wa 2021/22 kuanzia timu iliyoshika nafasi ya tatu hadi ya mwisho kulikuwa na tofauti ya alama mbili au tatu au moja tu ukiachilia Yanga SC na Simba SC ambapo walikuwa na tofauti ya alama zaidi ya kumi, hii ni kwa sababu ya maandalizi ndani ya vikosi vyao na zawadi kutoka kwa wadhamini zaidi ya mmoja".

Kwa upande wa kikosi cha Tanzania Prisons, Mtupa alibainisha wanafanya usajili kwa kuangalia wachezaji ambao watakuwa msaada ndani ya kikosi hicho.

"Kuhusu usajili kwa upande wetu bado tupo kwenye mawindo ya baadhi ya timu ili kupata wachezaji ambao watatuvusha malengo yetu".

# Polisi kuishtaki Singida, Mnata kwa TFF

Na Shufaa Lyimo

UONGOZI wa Timu ya Polisi Tanzania umesema unatarajia kupeleka barua Shirikisho la Soka Tanzania, TFF, kuishtaki Klabu ya Singida Big Stars United kwa kumsajili golikipa wao, Metacha Mnata ambaye bado hajamaliza mkataba na timu hiyo.

Akizuñgumza na gazeti hili jijini jana, Katibu Mkuu wa Timu ya Polisi, Michael Mtebene, alisema Metacha mkataba wake unamalizika msimu ujao.

"Metacha ni mchezaji wetu halali mkataba wake unamalizika msimu wa 202-2023 na jina lake lipo miongoni mwa wachezaji ambao msimu huu hatujawaacha hivyo tunampango wa kuiandikia TFF barua kuishitaki timu ya Singida Big Stars United kumsajili mchezaji wetu akiwa bado ana mkataba na sisi," alisema Mtebene.

Katibu huyo alisema hajapata taarifa au mawasiliano yoyote kutoka kwenye Uongozi wa Singida ukitaka kufahamu ukweli kuhusu mkataba wa Metacha.

"Singida walipaswa kufanya mawasiliano na sisi ili tuwaeleze ukweli kuhusu mkataba wa mchezaji huyo, lakini wameamua kuchukua maamuzi yao wenyewe ya kumsajili bila kufuata taratibu za mikataba," aliongeza.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### RONALDO AKATALIWA

MKURUGENZI wa Michezo wa Bayern Munich, Hasan Salihamidzic amesisitiza tena msimamo wa klabu hiyo ya Ujerumani kuhusu Cristiano Ronaldo, 37, kwa kukataa uwezekano wa kumnunua mshambuliaji huyo wa Manchester United na Ureno. ***(SPORT1 via Mail on Sunday)***

### BERNARDO HAUZWI

KLABU ya Manchester City haina nia ya kumuuza kiungo wa kati wa Ureno, Bernardo Silva, 27, kwenda Barcelona msimu huu wa joto, huku Kocha Pep Guardiola bado akimtazama mchezaji huyo kama sehemu muhimu ya mipango yake msimu ujao. ***(Sunday Mirror)***

### ZINCHENKO HUYO ARSENAL

KLABU ya Arsenal imekubali mkataba wa pauni milioni 30 kumsajili beki wa kushoto wa Ukraine, Oleksandr Zinchenko, 25, kutoka Manchester City. ***(Fabrizio Romano)***

### KOUNDE KUNUNULIWA

CHELSEA itamnunua beki wa kati wa Sevilla na Ufaransa, Jules Kounde, 23, baada ya kushindwa kuafikiana na Manchester City kwa ajili ya kumnunua mlinzi wa Uholanzi, Nathan Ake, 27. ***(Times)***

### HAG AKOMAA NA JONG

KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag ameuambia uongozi wa klabu hiyo kuendelea na majaribio yao ya kumsajili kiungo wa kati, Frenkie de Jong, 25, kutoka Barcelona. ***(Guardian)***

### GORDON AWINDWA

KLABU ya Everton imeanza mazungumzo juu ya mkataba mpya na mshambuliaji wa England, Anthony Gordon, 21, baada ya kukataa ofa ya pauni milioni 35 kwa mchezaji huyo kutoka Newcastle United. ***(Football Insider)***

### TANGANGA AWINDWA

KLABU ya AC Milan ipo kwenye mazungumzo na Tottenham Hotspur kuhusu kumsajili beki, Japhet Tanganga, 23. ***(Calciomercato)***

### MORATA KUSAJILIWA

KLABU ya Juventus imewasiliana na Atletico Madrid kuhusu kumsajili mshambuliaji wa Hispania, Alvaro Morata, 29, ambaye alirejea katika klabu hiyo msimu wa joto baada ya kumalizika kwa muda wa mkopo wa miaka miwili katika klabu hiyo ya Serie A. ***(Calciomercato)***


### CHUKWUEMEKA AWANIWA

PARIS St-Germain wameungana na Barcelona katika mawindo ya kumsajili kiungo, Carney Chukwuemeka, 18, kutoka Aston Villa. Mchezaji huyo aliachwa nje ya kikosi cha kocha Steven Gerrard kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya nchini Australia huku kukiwa na mvutano wa mkataba. ***(Sunday People)***

### JONES ATAKIWA

MLINZI wa Manchester United, Phil Jones, 30, analengwa na kocha mpya wa DC United, Wayne Rooney. ***(Daily Star Sunday)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# LEWANDOWSKI: ASANTE SANA BAYERN MUNICH

**Apanga siku ya kwenda kuwaaga baada ya kukamilisha ndoto yake kutua Barcelona...**

**MUNICH,** Ujerumani

ROBERT Lewandowski ametuma ujumbe wake wa kuwaaga mashabiki wa Bayern Munich Jumamosi, huku kukiwa na uthibitisho wa uhamisho wake wa hadhi ya juu kwenda Barcelona.

**Mchezaji huyo wa kimataifa wa Poland amesaini mkataba wa miaka minne na Barcelona, na hivyo kumaliza miezi kadhaa ya uvumi juu ya hatima yake.**

Mshindi huyo mara mbili wa kiatu cha Dhahabu cha Ulaya alikuwa amesisitiza nia yake ya kuondoka Bayern kufuatia mazungumzo ya muda mrefu ya kuongeza mkataba wake kugonga mwamba.

Huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 akitarajiwa kujiunga na kikosi cha Barcelona kwenye ziara yao nchini Marekani, alitoa shukrani zake kwa Bayern, ambapo alishinda taji la Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, katika kila misimu yake nane, pamoja na Ligi ya Mabingwa Ulaya na Klabu Bingwa ya Dunia.

"Ningependa kuwashukuru wachezaji wenzangu, wafanyakazi, usimamizi wa klabu na kila mtu ambaye amekuwa akiniunga mkono kila wakati na kutuwezesha kushinda mataji kwa FC Bayern," aliandika Lewandowski kupitia Instagram yake.

"Ninajivunia tulichofanikiwa pamoja. Zaidi ya yote, napenda kuwashukuru mashabiki kwa sababu ni nyinyi mnaifanya FC Bayern kuwa klabu maalum.

"Nina bahati kuwa na miaka nane ya ajabu na klabu hii na mashabiki wake na itabaki moyoni mwangu milele."

Akiwa ameifungia Bayern mabao 344 katika mechi 375 kwenye michuano yote, Lewandowski anakuwa mchezaji wa nne kusajiliwa na Barcelona msimu huu licha ya matatizo ya kifedha yanayotangazwa na klabu hiyo, akiungana na Franck Kessie, Andreas Christensen na Raphinha.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 288

MECHI KALI
BORUSSIA DORTMUND
VERSUS
VELENCIA
1 | 1.82
X | 3.69
2 | 3.59

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# RONALDO AKATALIWA BAYERN



**MUNICH,** Ujerumani

MKURUGENZI wa Michezo wa Bayern, Munich Hasan Salihamidzic amesisitiza tena kwamba, klabu hiyo haitamsajili Cristiano Ronaldo msimu huu wa joto, licha ya mshambuliaji nyota Robert Lewandowski kuondoka hapo.

Kama ilivyoripotiwa na 90min, Barcelona wamekubali dili la euro milioni 50 na Bayern kwa huduma ya Lewandowski, huku La Blaugrana hao wakikamilisha uhamisho huo jana Jumapili.

Kuondoka kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Poland kutaiacha Bayern ikiwa na pengo kubwa mbele, na wamehusishwa na Ronaldo hivi majuzi.

Hata hivyo, kwa mara nyingine, wale walio juu ya klabu hiyo wamekataa kabisa mshambuliaji huyo wa Manchester United kujiunga na Bayern msimu huu wa joto.

"Ninamheshimu sana Cristiano Ronaldo, mafanikio yake na kazi yake. Lakini kwa mara nyingine tena: Hiyo ilikuwa na sio mada kwetu," alisema Salihamidzic akiiambia Sport.

"Hatujawahi kuzungumza kuhusu kumsajili Ronaldo, na wala hata wakala hatuna mipango hiyo kwa sasa."

90min inaelewa kuwa Ronaldo ameomba United kuzingatia ofa zozote zinazofaa kwa huduma yake msimu huu wa joto.



## De Jong agoma kuhamia Man U

**BARCELONA,** Hispania

UHAMISHO wa Frenkie de Jong wa Barcelona kwenda Manchester United huenda ukashindikana ingawa Barcelona imekubali ombi la klabu hiyo ya Ligi Kuu England.

Ripoti ya gazeti la kila siku Sport la Hispania imesema wakala wa kiungo huyo wa Uholanzi, Ali Dursun amekutana na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Man United, Richard Arnold na Mkurugenzi wa michezo wa klabu hiyo John Murtough na kukataa ombi lao.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo De Jong hakatai kuondoka Barcelona msimu huu, lakini ameweka msimamo hataki kwenda Manchester United.

Barca inataka kumuuza De Jong mwenye umri wa miaka 25 ili kupata fedha zaidi hasa kutokana na sasa kuwa kwenye matatizo ya kiuchumi.

De Jong mara kadhaa amesisitiza kuwa hataki kwenda nchini England kwa sababu yeye anataka kubakia Katalunya.

Mapema wiki iliyopita alinukuliwa akisema kwamba, hali ya hewa na nchini England sio rafiki kwake na tayari ameshanunua jumba la kifahari pale Katalunya.

## HABARI MICHEZO


,541,640

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 20/07/22 | 18:00 | CA Fenix vs Mvo Wanderers | 2.39 | 3.02 | 3.12 |
| 02. 20/07/22 | 20:00 | Maccabi Haifa vs Olympiakos | 3.16 | 3.11 | 2.37 |
| 03. 20/07/22 | 20:00 | San Lorenzo vs Union Santa Fe | 2.44 | 3.18 | 3.07 |
| 04. 20/07/22 | 20:00 | Botev Plovdiv vs Apoel Nicosia | 2.88 | 3.23 | 2.42 |
| 05. 20/07/22 | 21:00 | Dynamo Kiev vs Fenerbahce | 2.75 | 3.30 | 2.55 |
| 06. 20/07/22 | 21:15 | Maribor vs Sheriff Tiraspol | 2.79 | 3.09 | 2.64 |
| 07. 21/07/22 | 01:00 | Goias vs Fluminense | 3.24 | 3.19 | 2.26 |
| 08. 21/07/22 | 01:00 | CSA AL vs Cruzeiro | 3.18 | 2.93 | 2.41 |
| 09. 21/07/22 | 01:00 | Defensa Justicia vs Independiente | 2.30 | 3.23 | 3.28 |
| 10. 21/07/22 | 02:30 | Internacional vs Sao Paulo | 2.34 | 3.14 | 3.14 |
| 11. 21/07/22 | 03:30 | Lanus vs Velez Sarsfield | 2.82 | 3.12 | 2.67 |
| 12. 21/07/22 | 05:05 | Guadalajara Chivas vs Club Leon | 2.26 | 3.24 | 3.19 |
| 13. 21/07/22 | 20:30 | Aris Limassol vs Neftchi Baku | 2.37 | 3.16 | 3.01 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 18/07/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 2199 | Busan I Park vs Ansan Greeners | 1.92 | 3.29 | 3.64 |
| 13:00 | 3334 | Saif SC vs Bashundhara Kings | 3.00 | 3.35 | 2.22 |
| 13:00 | 3816 | Roasso Kumamoto vs Renofa Yamaguchi | 1.99 | 3.19 | 3.53 |
| 13:30 | 1383 | Daejeon Citizen vs Seoul E Land | 1.83 | 3.44 | 3.83 |
| 16:00 | 1340 | Boca Jrs vs Argentinos Juniors Reserve | 2.05 | 3.29 | 3.24 |
| 17:00 | 3080 | Banfield Reserve vs CA Talleres de Cordoba Reserve | 2.05 | 3.15 | 3.40 |
| 17:00 | 3759 | CA Sarmiento de Junin vs Atletico Tucuman Reserve | 2.44 | 3.19 | 2.65 |
| 17:00 | 3777 | Newells Old Boys vs Rosario Central Reserve | 2.50 | 3.18 | 2.60 |
| 17:00 | 3842 | Mainz vs Newcastle | 4.20 | 3.75 | 1.73 |
| 17:00 | 5193 | Sotra vs Odds BK 2 | 1.87 | 4.12 | 3.09 |
| 18:00 | 1950 | FK Auda vs FK Tukums 2000/Tss | 1.37 | 4.40 | 7.04 |
| 18:00 | 3488 | Haka vs Inter Turku | 2.38 | 3.18 | 2.74 |
| 18:30 | 3618 | Hebar Pazardzhik vs Septemvri Sofia | 2.24 | 3.13 | 2.99 |
| 18:30 | 3641 | FK CSKA 1948 II vs Yantra Gabrovo | 1.56 | 3.78 | 5.11 |
| 18:30 | 5046 | Toten vs Aalesund 2 | 12.75 | 7.85 | 1.12 |
| 18:30 | 5642 | Botosani vs Chindia Targoviste | 2.07 | 3.05 | 3.70 |
| 19:00 | 1393 | Harju JK Laagri vs Flora II | 1.76 | 3.99 | 3.99 |
| 19:00 | 1533 | Raufoss vs Brann | 5.50 | 4.52 | 1.43 |
| 19:00 | 2069 | Aasane Fotball vs Skeid Fotball | 1.97 | 3.59 | 3.20 |
| 19:00 | 2278 | Grorud IL vs Mjondalen | 2.64 | 3.42 | 2.33 |
| 19:00 | 2839 | Valerenga IF 2 vs Gjovik-Lyn | 2.45 | 3.73 | 2.36 |
| 19:00 | 3378 | Bryne vs Fredrikstad | 2.30 | 3.30 | 2.76 |
| 19:00 | 3435 | Belshina vs Shakhter Soligorsk | 6.67 | 4.22 | 1.40 |
| 19:00 | 3542 | Paide Linnameeskond vs FCI Levadia Tallinn U21 | 8.24 | 6.83 | 1.25 |
| 19:00 | 3610 | Zaglebie Sosnowiec vs Resovia Rzeszow | 2.25 | 3.24 | 2.89 |
| 19:00 | 4778 | IK Start vs Sandnes Ulf | 1.55 | 4.03 | 4.81 |
| 19:00 | 5021 | FC Nomme United vs Viljandi Tulevik | 1.27 | 6.28 | 8.30 |
| 19:30 | 1212 | Misr Lel Makasa vs Enppi Club | 4.43 | 3.07 | 1.91 |
| 19:30 | 3561 | Farco FC vs Eastern Company SC | 1.98 | 3.17 | 3.92 |
| 20:00 | 1848 | Zambia W vs South Africa W | 3.50 | 3.11 | 2.03 |
| 20:00 | 2209 | Gornik Zabrze vs Cracovia | 2.20 | 3.15 | 3.05 |
| 20:00 | 2426 | TUS Heiligenkreuz vs SC Kalsdorf | 2.55 | 4.20 | 2.21 |
| 20:00 | 2689 | GIF Sundsvall vs BK Hacken | 4.91 | 4.32 | 1.50 |
| 20:00 | 3013 | Odense vs Nordsjalland | 2.12 | 3.47 | 3.17 |
| 20:00 | 3061 | AFC Eskilstuna vs Trelleborgs FF | 2.49 | 3.63 | 2.61 |
| 20:00 | 3428 | Pachuca U20 vs Mazatlan FC U20 | 1.63 | 4.10 | 4.50 |
| 20:00 | 3553 | Varbergs Bois vs Helsingborg | 2.04 | 3.28 | 3.28 |
| 20:00 | 3651 | FC Alania Vladikavkaz vs FC Dynamo-Makhachkala | 1.39 | 4.33 | 6.70 |
| 20:00 | 4992 | Borussia Dortmund vs Valencia | 1.82 | 3.69 | 3.59 |
| 20:00 | 5091 | FK Haugesund 2 vs Vidar | 6.10 | 5.31 | 1.34 |
| 20:45 | 2326 | Arda Kurdzhali vs Beroe | 2.80 | 3.15 | 2.35 |
| 21:15 | 4481 | ND Gorica vs ASK Bravo | 3.09 | 3.24 | 2.14 |
| 21:30 | 3303 | Petrolul Ploiesti vs Voluntari | 2.51 | 2.96 | 2.91 |
| 21:30 | 4199 | Atyra FC vs Fernando Mora | 3.83 | 2.99 | 1.98 |
| 22:00 | 4397 | Iceland W vs France W | 7.45 | 4.90 | 1.31 |
| 22:00 | 5077 | Italy W vs Belgium W | 1.99 | 3.39 | 3.29 |
| 22:00 | 5319 | El Ittihad Alexandria vs Al Masry Club | 2.49 | 3.02 | 2.92 |
| 23:00 | 1802 | Morocco W vs Nigeria W | 3.87 | 3.14 | 1.91 |
| 23:30 | 2195 | UTC Cajamarca vs Alianza Atletico | 1.82 | 3.49 | 3.79 |
| 23:45 | 2044 | Puebla FC W vs Unam W | 3.14 | 3.78 | 1.93 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# PBZ KUDHAMINI LIGI KUU ZANZIBAR MIAKA MITANO

**Na Hawa Abdallah, Zanzibar**

BENKI ya Watu wa Zanzibar, PBZ imetiliana saini na Shirikisho la Mpira wa Miguu la Zanzibar, ZFF, kuendelea kudhamini Ligi Kuu ya visiwani humo kwa miaka mitano.

Udhamini huo wenye thamani ya Shilingi bilioni tatu, milioni mia tano na laki tano utaanza rasmi msimu huu mpya wa 2022-2023.

Hafla hiyo ya utiaji saini ilifanyika usiku wa tuzo za Ligi Kuu ya Zanzibar mwishoni mwa wiki.

**Akizungumza na gazeti hili Rais wa ZFF, Abdulatif Ali Yasini, alisema hii ni hatua kubwa ya kufungua milango kwa wafanyabiashara mbalimbali kwenda kuwekeza katika soka la Zanzibar.**

Alisema Ligi Kuu ya Zanzibar itaendelea kudhaminiwa na PBZ kwa miaka mitano na anamatumaini makubwa kutoka kwa timu zote zitakazoshiriki.

Alisema kuwa PBZ kuendelea kudhamini Ligi ya Zanzibar ni baada ya mafanikio yaliyopatikana katika msimu uliomalizika.

"Tunaishukuru serikali kwa kuendelea kusimamia mpira wa miguu wa Zanzibar hasa katika kutoa nguvu yao kubwa juu ya kupata udhamini wa ligi, hii ni fursa ambayo tunatakiwa kuitumia vizuri na kufikia malengo," alisema.



Wachezaji wa timu ya mpira wa Netiboli ya JKT Mbweni, (jezi za njano), wakimiliki mpira huku wakizongwa na mchezaji wa timu ya UDSM, katika michuano ya mchezo huo inayofanyika kwenye Uwanja wa Ndani wa Taifa, Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**



# *Nandy kutaja wasanii wa tamasha lake*

**Na Sabato Kasika**

NYOTA wa muziki wa kizazi kipya Nandy, amesema wakati wowote kuanzia sasa ataweka hadharani majina ya wasanii watakaoshiriki katika tamasha lake la 'Nandy Festival'.

Tamasha hilo lenye kaulimbiu ya 'Tupo Veree', linatarajiwa kufanyika Julai 23, mwaka huu, katika Uwanja wa Majimaji mjini Songea mkoani Ruvuma likishirikisha wasanii wengi wa ndani na wengine kutoka nje ya nchi.

Wiki iliyopita, msanii huyo alikaririwa na vyombo vya habari akisema kuwa anasubiri kwanza afunge ndoa ndipo aweke hadharani majina ya wasanii hao.

Tayari ameshafunga ndoa na msanii mwenzake Billnass na sasa kilichobaki ni kutangaza majina ya wasanii hao watakaosaidia kufanikisha tamasha hilo ambalo safari hii atalifanya akiwa ni mke wa mtu.

Nandy alikaririwa akisema kuwa pamoja na kwamba ni mjamzito, atashiriki kama kawaida katika tamasha hilo.

"Wale ambao wanadhani kwamba mimba inaweza kunikwamisha, waje washuhudie jinsi nitakavyofanya kazi," alisema Nandy.

Michezo
Jumatatu Julai 18, 2022
Nipashe



Lewandowski: Asante Bayern
UKURASA 21

# Simba SC kucheza mechi tano Misri

## ●●● Phiri ajiunga na wenzake, wapya wiki ijao...

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Simba, Zoran Maki (pichani) amesema wanaendelea vema na mazoezi magumu ya maandalizi ya mwanzo wa msimu, huku akitarajia timu yake kucheza mechi nne au tano za kirafiki.

**Akizungumza kutoka Ismailia nchini Misri, kocha huyo mwenye uraia pacha wa Serbia na Ureno, alisema mbali na kufanya mazoezi ya kuweka miili fiti, lakini anataka kuangalia viwango vya baadhi ya wachezaji, ingawa baadhi yao anafahamu habari na uwezo wao kidogo.**

"Mazoezi ni mazuri, najua kidogo habari na uwezo wa baadhi ya wachezaji niliokuwa nao hapa, lakini nataka niangalie viwango vyao. Tukiwa hapa tutacheza mechi nne au tano za kirafiki na hii ni kwa ajili ya kupima uwezo wetu ulivyo na kujipima kama bado tupandishe kiwango au kimefikia pale tunapotaka," alisema kocha huyo.



Kocha huyo amewapongeza viongozi wa Simba na klabu kwa ujumla kwa kumletea msaidizi ambaye ni Sbai Karim akija kuhudumu kama kocha msaidizi na viungo pia.

"Hii ni muhimu sana kwa nyakati hizi za mwanzo wa msimu kuwa naye, nafikiri atajiunga na sisi baada ya kesho (leo). Wameniambia kuna wachezaji watano watafika, lakini kuna wachezaji wapya watatangazwa, ni vizuri wakija haraka kwa sababu ya kutengeneza mfumo," alisema.

Wakati kocha huyo akizungumza hayo, tayari kundi la pili la wachezaji watano limewasili nchini humo jana, akiwamo straika mpya Moses Phiri ambaye alikwama kutokana na masuala ya viza.

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally alisema wachezaji waliotarajiwa kuwapokea jana mbali na Phiri ni Enock Inonga, Peter Banda, Thadeo Lwanga na Nassor Kapama.

"Tunawapokea wachezaji wetu watano wanaokuja kuungana nasi kwenye maandalizi ya mwanzo wa msimu, mchezaji Saido Kanoute atajiunga nasi wiki ijayo akitokea kwao nchini Mali baada ya kukamilisha mipango ya viza," alisema Ahmed.

Kuhusu wachezaji wapya, meneja huyo alisema wiki ijayo watatangaza wachezaji watatu wapya ambao imewasajili kwa msimu ujao wa ligi.

"Wachezaji watatu wapya ambao ni usajili mpya tutawatangaza wiki ijayo na watajiunga nasi wiki hiyo hiyo."

Hii inaweza kuwa ni faraja kwa wanachama na mashabiki wa Simba ambao walikuwa na sintofahamu baada ya ukimya wa kutotangaza tena usajili baada ya ule wa Augustine Okra kutoka Ghana.

Baadhi ya tetesi zikidai kuwa ndiyo imeshamaliza, huku zingine zikidai klabu hiyo imesitisha kusajili kutokana na mapendekezo ya kocha akitaka kwanza kuwaangalia wachezaji waliopo, jambo ambalo lilionekana kutowafurahisha wengi kwa madai huu si wakati tena wa kuwaangalia wachezaji ambao wameshuka viwango na kushindwa kuipa timu mataji.



Wachezaji wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Mzamiru Yassin na Bakari Mwamnyeto wakiwa kwenye mazoezi katika Uwanja wa JKM Park kujiandaa na michezo ya kufuzu CHAN 2023 dhidi ya Somalia itakayochezwa Julai 23, 2022 na Julai 30, 2022. **PICHA:TFF**

# TFF yafungia viwanja saba

**Na Adam Fungamwango**

BODI ya Ligi Kuu Tanzania Bara imevipiga 'stop' viwanja saba vilivyokuwa vinatumika kwenye ligi msimu uliopita hadi hapo vitakapofanyiwa marekebisho.

Viwanja vilivyosimamishwa hadi hapo vitakapofanyiwa marekebisho, la sivyo havitotumika kwa msimu ujao wa Ligi Kuu 2022/23 ni Mkwakwani Tanga, Ilulu Lindi, Ushirika Kilimanjaro, Mabatini Pwani, Sokoine Mbeya, Jamhuri Dodoma na Nyankumbu Girls, Geita.

Taarifa iliyotolewa jana na Idara wa Habari na Mawasiliano ya Bodi hiyo imesema kuwa wakati unasubiri taarifa ya ukaguzi wa viwanja unaofanywa na Kamati ya Leseni za Klabu iliyo chini ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), imefanya tathmini ya viwanja vilivyotumika kwenye mechi za Ligi Kuu msimu uliomalizika na kubaini mapungufu kadhaa kwenye viwanja hivyo.

Taarifa hiyo imebainisha jumla mapungufu 10 ambayo yapo kwenye viwanja hivyo, kila uwanja ukiwa na mapungufu yake kadhaa, hivyo Bodi ya Ligi imezitaka klabu zinazotaraji kutumia viwanja hivyo kufanya jitihada za makusudi katika kuboresha maeneo yalioainishwa ili kukidhi matakwa ya kanuni na sheria zinazoongoza mpira wa miguu.

Baadhi ya mapungufu yalioainishwa kwenye viwanja hivyo ni eneo la kuchezea kutokuwa tambarare na kukosa nyasi za kutosha, pili ni ubovu katika uzio wa kutenganisha mashabiki na eneo la kuchezea, tatu vyumba vya kuvalia nguo za wachezaji na waamuzi kukosa sifa nne ambazo zimeainishwa pia.

Bodi ya Ligi imetaja mapungufu mengine kuwa ni kukosekana majukwaa kwa ajili ya watazamaji, kukosekana kwa chumba cha madaktari kwa ajili ya huduma ya kwanza, pia chumba cha mawasiliano.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002